# Nipashe

Jumatano Mei 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580935

www.ippmedia.com

MWANGA WA JA...

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 70071...

LIKE & FOLLOW






SportPesa

TZS. 1,224,601,040

BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Hoja** nne kuteka mjadala Wizara Mambo ya Ndani

UKURASA 4

**REAL MADRID KUIVAA MAN CITY BILA ALABA**

UKURASA 22



"Hata bajeti yetu itakuwa na manufaa kama serikali itapata takwimu sahihi za wananchi wake.

**SHEKHE DODOMA**



"Serikali ya Saud Arabia imetangaza nafasi za mahujaji milioni moja kwa Watanzania wanaotaka kwenda kufanya ibada ya Hijja mwaka huu.

**DK. MWINYI**



"Hili ni jambo letu sote msifuate kauli au yanayosemwa katika Uislamu hakuna Sensa. Sensa ipo mwaka huu na serikali imeweka utaratibu mzuri.

**MUFTI**

## SALAMU ZA EID

# Mashekhe wapaza sauti dhidi ya mauaji kikatili

• **Wasisitiza** amani na upendo, sensa, Dk. Mwinyi atangaza habari njema Hijja... *Endelea ukurasa 2 & 3*




Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia wadau mbalimbali wa sekta ya habari katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# ACT yaja na hatua tatu kuwakabili 'panya road'

UKURASA 4

# Samia awapa wanahabari hoja nne wazifanyie kazi

UK. 3


**MICHEZO** **SIMBA YAISOGEZEA UBINGWA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mashekhe wapaza sauti za mauaji ya kikatili Eid

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini ya Kiislam wamepaza sauti dhidi ya mauaji ya kikatili huku wakihamasisha waumini wa dini hiyo na wananchi wengine kujitokeza kushiriki sensa ya watu na makazi iliyopangwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Mkoani Katavi jana wakati wa sala ya Eid, Shekhe wa Mkoa huo, Mashaka Kakulukulu, alisema Eid ni siku ya kumtukuza Mungu na siyo siku ya kumuasi, akionya kuwa kuasi Eid ni sawa na kuasi siku ya hukumu.

Shekhe Kakulukulu alikemea mauaji ya kikatili yanayoendelea kutokea katika sehemu mbalimbali nchini, akisisitiza kuwa adhabu ya mtu anayemuua mtu mwingine iko mbele ya Mungu.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni kukosa hofu ya Mungu, hivyo akamtaka kila mmoja kuwa na hofu ya Mungu na kuwa balozi mzuri kwa mtu mwingine.

"Tunamwomba Mungu asitunyime malipo ya funga tulizofunga, Mwenyezi Mungu amekemea watu kutoshikamana kuwa kitu kimoja, hivyo tupendane, tushikamane na dini zote, amani haiwezi kupatikana kama upendo haupo," alisema Shekhe Kakulukulu.

**SENSA 2022**

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, wakati wa sala ya Eid El Fitri jana kwenye Msikiti wa Gadafi, alihimiza wananchi kushiriki sensa ya watu na makazi kwa kuwa serikali inakwenda kutekeleza tukio muhimu.

"Sensa ni muhimu sana kwa taifa letu, lazima wote tuhakikishe kuwa tunahesabiwa lakini kutoa ushirikiano kwa serikali ili kufanikisha suala hili muhimu.

"Hata bajeti yetu itakuwa na manufaa kama serikali itapata takwimu sahihi za wananchi wake, hivyo wote tushiriki kuhesabiwa au kutoa ushirikiano wa kila hali kwa wataalamu wa zoezi hili ili serikali kupata takwimu sahihi zitazosaidia kufikisha maendeleo kwa wananchi wake," alisema.

Shekhe huyo alisema Watanzania wanapaswa kuendelea kushirikiana bila kujali makabila, dini au rangi zao na kuitunza amani iliyopo.

Shekhe wa Mkoa wa Mbeya, Msafiri Njalabaha, aliwataka waumini wa dini hiyo kujiandaa kuhesabiwa na kuhakikisha wanatoa taarifa sahihi kwa maofisa watakaokwenda kuwahesabu ili kuliwezesha Taifa kuwa na takwimu sahihi za wananchi wake.

Alisema sensa ina manufaa kwa Taifa na kwamba zoezi hilo siyo haramu kwa mujibu wa dini ya Kiislamu kwa kuwa limeandikwa hata kwenye maandiko matakatifu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema maandalizi kwa ajili ya sensa yamekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na sasa wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wote washiriki zoezi hilo.

Mkoani Shinyanga, Shekhe wa Mkoa huo, aliwataka Watanzania kuendelea kudumisha amani ya nchi pamoja na kumwombea afya njema Rais Samia Suluhu Hassan ili alitumikie Taifa vizuri na kuleta maendeleo.

Shekhe Ismail Makusanya wakati wa sala ya Eid EL-Fitri kwenye viwanja vya michezo vya Sabasaba mjini Shinyanga jana, alisema waumini wa dini ya Kiislamu na Watanzania wote kwa ujumla wanapaswa kuendelea kudumisha amani ya nchi, kuwa na upendo, utulivu, kushikamana na kumwombea Rais Samia aendelee kuwa na afya njema na kuliongoza Taifa vizuri.

"Waislamu tunapoherehekea sikukuu hii ya Eid, tuwakumbuke yatima, wajane, wafungwa na watu wenye ulemavu kwa kuwapatia misaada mbalimbali ili tupate thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu," alisema.

Shekhe Tamimu Saidi katika sala ya Eid El Fitri wilayani Muheza alisema Waislam wote na Watanzania kwa ujumla wamepaswa kuendelea kuonyesha upendo, umoja na kuvumiliana hasa baada ya kumalizika kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema wananchi wanaposherehekea sikukuu ya Eid El Fitri waendelee kudumisha amani na utulivu kwa kujiepusha na vitendo vibaya vinavyoashiria vurugu, uonevu na uvunjifu wa amani kwa kuwa havina tija.

**KILIMO**

Mjini Moshi jana Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Kilimanjaro liliomba serikali kupitia wataalamu wa kilimo kuwaelimisha wananchi kupanda mazao yanayokomaa haraka na yanayostahimili ukame ikiwamo muhogo ili kuendana na hali ya mvua ya mwaka huu.

Shekhe wa Mkoa wa Kilimanjaro, Shaabani Mlewa, akizungumza na waumini wa dini ya kiislam katika Msikiti wa Riadha, aliiomba serikali kupitia maofisa kilimo kutembelea wakulima na kuwapa elimu ya kupanda mazao ya muda mfupi na yanayostahimili ukame.

"Ni kweli kutoa elimu ni wajibu wao. Kwa sasa kila mtu amejionea baadhi ya wilaya zetu hali siyo nzuri ya mazao, ndiyo maana nimeona niombe maofisa hao wanaingia vijijini na kutoa elimu hasa kwenye zile wilaya ambazo hali ya mazoea siyo nzuri. Pia kuhimiza wananchi kuhifadhi vyakula na kuacha kuuza kwa mambo yasiyokuwa na msingi," alisema.

**MSHIKAMANO**

Jijini Mwanza, Shekhe wa Mkoa huo aliwataka waumini wa dini ya Kiislam kuwa na mshikamano na kuepuka baadhi ya itikadi zinazowatenganisha.

Akihutubia mamia ya waumini hao katika viwanja vya Nyamagana, Shekhe Hasani Kabeke, alisema waumini hao wanatakiwa kubaki katika imani na mshikamano.

Shekhe wa Mkoa wa Pwani, Khamis Mtupa, aliungana na viongozi wake kuwataka waumini wa dini ya Kiislamu kuhakikisha wanajitokeza kwenye sensa Agosti mwaka huu kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi za idadi ya watu ambayo itasaidia wakati wakipanga bajeti zao.

Shekhe Mtupa alisema utaratibu wa sensa upo kwa miaka mingi na hata kwenye maandiko upo, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuwa tayari kushiriki zoezi hilo.

Alisema serikali haliwezi kupanga bajeti yake vizuri bila kuwa na takwimu sahihi, hivyo wananchi wanatakiwa kuwa tayari kwa manufaa ya maendeleo ya nchi.

***Imeandikwa na Neema Hussein (KATAVI), Paul Mabeja (DODOMA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Steven William (MUHEZA), Nebart Msokwa (MBEYA), Anjela Mhando (MOSHI), Julieth Mkireri (KIBAHA) na Vitus Audax (MWANZA).**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Mwinyi, akitoa mkono wa Eid El Fitr kwa watoto waliofika katika viwanja vya Ikulu jijini Zanzibar jana. Picha zaidi **Uk. 18. PICHA: IKULU**

# Mufti ahimiza ushiriki sensa

**Na Jenifer Gilla**

MUFTI wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeir, amewataka waumini wa dini ya Kiislamu kujitokeza kushiriki katika Sensa na Makazi itakayofanyika Agosti 23 mwaka huu.

Shekhe Zubeir alitoa rai hiyo jana katika sala ya Eid El- Fitr iliyofanyika kitaifa katika Msikiti wa Mfalme Mohamed VI ulioko Kinondoni, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na viongozi wengine wa kitaifa.

"Hili ni jambo letu sote msifuate kauli au yanayosema katika Uislamu hakuna sensa. Sensa ipo mwaka huu na serikali imeweka utaratibu mzuri. Ni jukumu letu viongozi wa dini kuwajibika kwa kuwaambia Waislamu na Watanzania kushiriki mchakato huu," alisema Shekhe Zubeir.

Aliwataka Waislam na Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki suala hilo kwa kuwa ni haki kwa Waislamu na Watanzania kushiriki na kukubali kuhesabiwa kwa manufaa ya Taifa.

Mufti huyo pia aliwataka waumini kuwa na umoja na mshikamano miongoni mwao ikiwamo kuwa na undugu dhidi ya Watanzania.

"Tuwe na umoja na tujenge undugu zaidi, kila mmoja amuone mwenzake ni ndugu na jamaa yake wa karibu ambaye ana haki ya kuheshimu," alisema.

Katibu wa Baraza la Ulamaa la Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Shekhe Hassan Chizenga, aliwataka waumini hao kuendelea kutenda mema waliyokuwa wanayafanya katika mwezi mzima wa Ramadhani, ikiwamo kuwa na tabia njema na kutoa sadaka.

"Endeleeni kutoa zawadi na tabia njema kwa kila binadamu na ulimwenguni kote. Sambazeni zawadi hizi ili viongozi wote waonekane kwa tabia njema mlizozipata ndani ya Mwezi Mtukufu," alisema Shekhe Chizenga.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Tanzania mwaka jana ilikadiriwa kuwa na watu 59,441,988 (milioni 59.442). Kati yao, wanaume ni 29,132,238 na wanawake 30,309,750.

**SENSA TANZANIA**

| Mwaka | Idadi ya watu | Tanzania Bara | Zanzibar |
|---|---|---|---|
| 1967 | 12,313,469 | 11,958,654 | 354,815 |
| 1978 | 17,512,610 | 17,512,610 | 476,111 |
| 1988 | 23,095,878 | 22,455,193 | 640,685 |
| 2002 | 34,569,232 | 33,584,607 | 984,625 |
| 2012 | 44,928,923 | 43,625,354 | 1,303,569 |

**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)**

## Saudia yafungua milango Hijja, Watanzania milioni moja kwenda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SAUDI Arabia imefungua milango ya ibada ya Hijja kwa waumini wa dini ya Kiislamu kuanzia mwaka huu baada ya kusimamisha kutokana na janga la ugonjwa wa UVIKO- 19 lililokuwa limeiandama dunia.

Kutokana na kufunguliwa kwa milango hiyo kwa ajili ya Hijja ambayo ni moja ya nguzo tano za dini ya Kiislamu, Watanzania milioni moja wanatarajia kuhudhuria kutokana na kibali kilichotolewa.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema hayo jana katika Baraza la Eid el Fitri lililofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdul Wakil, Kikwajuni kisiwani hapo.

Kutokana na hatua hiyo, Rais Dk. Mwinyi aliishukuru serikali ya Saudi Arabia kuruhusu Watanzania kwenda kufanya ibada hiyo muhimu.

"Serikali ya Saudi Arabia imetangaza nafasi za mahujaji milioni moja kwa Watanzania wanaotaka kwenda kufanya ibada ya Hijja nchini humo kwa mwaka huu. Hii ni taarifa njema sana kwa Waislamu," alisema.

Dk. Mwinyi alisema alisema nafasi hizo zilizotangazwa kwa Watanzania zinatosheleza kwa Waislam wenye nia na uwezo wa kutekeleza ibada hiyo.

Alisema serikali yake itatoa ushirikiano kwa mahujaji watarajiwa ili kwenda kutimiza nguzo hiyo muhimu ya Kiislamu kwa kila mwenye uwezo.

Pia alisema anatambua mitihani ambayo Waislam wa Tanzania na sehemu zingine duniani wameshindwa kwenda katika ibada ya Hijja kutokana na kuzuka kwa janga la UVIKO-19.

Katika kusherehekea sikukuu ya Eid el Fitri, Dk. Mwinyi aliitaka Jeshi la Polisi kuongeza nguvu katika kusimamia usalama barabarani ili kupunguza ajali na msongamano wa magari.

Pia aliwataka madereva wa vyombo vya usafiri barabarani kuwa makini na kufuata sheria za barabarani ili kuepukana na ajali zisizo za lazima.

Kadhalika, aliwataka wazazi na walezi kuzingatia usalama wa watoto kwa kuwasimamia ili kuwa salama muda wote.

Kabla ya baraza hilo, Dk. mwinyi aliwaongoza Waislamu katika ibada maalum ya sala ya Eid katika Msikiti Zinjibar, Mazizini Zanzibar. Ibada hiyo ilifanyika baada ya kukamilika kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.




Madareva wa bodaboda wakisubiri kuvuka makutano ya Barabara ya Bagamoyo na Sam Nujoma Mwenge, mkoani Dar es Salaam juzi, huku wakiwa wamevuka alama za pundamilia, kitendo ambacho ni kinyume na sheria ya usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia awapa wanahabari hoja nne wazifanyie kazi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameendelea historia ya ubia na waandishi wa habari, alipohudhuria tukio lao la kimataifa na kuwaachia hoja nne anazoamini ndiyo msingi wa tija.

Akiwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, Tanzania ikiwa mwenyeji wa tukio barani Afrika jijini hapa jana iliyoendana na shamrashamra za Eid El Fitri, alizitaja hoja hizo ni miiko, sheria, kujifunza na uzalendo.

Katika hotuba yake iliyogeuka kivutio, huku akisimama kwa nafasi ya rafiki na mdau wa wanataluma hao, baadhi akiwatambua hata kwa majina na mawasiliano binafsi ikiwamo ya karibuni, Rais alikosoa taaluma hiyo kwamba inakosa baadhi ya vigezo vya ufanisi.

Rais Samia pia alikosoa kwa kina kwa aliyoyatambua kuwa ni udhaifu uliokithiri ndani ya mitandao ya hifadhi ya jamii, huku katika sura ya pili akiungana na waandishi wa habari kwenye kilio chao cha marekebisho ya sheria kwamba kinafanyiwa kazi.

Alifafanua kwamba alishaagiza kuwa Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 inayolalamikiwa na wanafani hao ifanyiwe marekebisho kwa kuanzia kwenye majadiliano, hatua iliyothibitishwa awali na Waziri mwenye dhamana, Nape Nnauye.

Hata hivyo, aliweka angalizo alilolitamka kuwa ni 'busara itangulie kwa wahusika'. Alieleza: "Nimeagiza sheria na kanuni za kihabari kupitiwa na kufanyiwa marekebisho, lakini kwa kufanya majadiliano kwa kuwa uhuru unatakiwa kuwapo, lakini kuna mipaka yake."

Kuhusu mitandao ya kijamii, Rais Samia alilalamika: "Wapo watu wanatumia vibaya vyombo vya habari, hasa katika mitandao ya kijamii kwa kuwa wanafahamu kuna sheria na mikataba ya kimataifa.

"Hakuna kizuri kama kujilinda mwenyewe hata kama umepewa fedha uandike habari fulani, chukua fedha hizo lakini kabla ya kufanya hivyo fikiria kwanza.

"Lazima tulinde mila na desturi zetu za Kiafrika, ili kuepuka migongano kwa kuwa wapo watu wanatumia vibaya mitandao ya kijamii kuweka maudhui ambayo ni yanakwenda kinyume cha mila, desturi na utamaduni wa Kiafrika."

Rais Samia ambaye muda mrefu alitumia mfumo wa kufundisha na kushauri, alihimiza uzingatiaji sheria, akiwa na angalizo lake 'hakuna haja ya waandishi kulumbana na serikali ilhali wanajenga nchi moja'.

Akiendeleza ufafanuzi wake, aliwakumbusha wanahabari nafasi ya sheria na mamlaka zilizo juu yao, akitumia tamathali "Ukinikuna na mimi nitakupapasa, ukinikwarua na mimi nitakuparura kwa kuwa sheria bado zipo na hazijabadilika."

Rais Samia aliwakumbusha waandishi wa habari kuwa makini mbali na kutumika kuandika yanayokinzana na maisha yao kisheria, kimantiki na kimaadili.

Vilevile, aliwataka wakimbizane na mahitaji ya kielimu ikiwamo kuvitumia vyombo wafadhili, akitoa mfano UNESCO kujizatiti kitaaluma, huku akiwarejea kuwakosoa uandishi wao ubebe ujumbe wenye mantiki inayoendana na ukweli uliopo.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nnauye, alisema kutokana na agizo la Rais wameshaanza kufanya mapitio ya sheria na kanuni zinazolalamikiwa na waandishi wa habari.

Aliwataka waandishi wa habari kutumia busara ili wafike salama katika kipindi cha mpito hadi kukamilika kwa mabadiliko ya sheria hizo.

"Kutokana na sheria hizo kuwa bado zipo tuende kwa busara ili tufike salama na pamoja katika kipindi hiki cha mpito kwa kuwa mapitio yamelenga kuboresha tasnia ya habari, maslahi ya waandishi na kujisimamia wenyewe.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jim Yonazi, alisema wizara hiyo na waandishi wa habari nchini wanampongeza Rais Samia kwa kuwapa ushirikiano katika sekta hiyo.

Alisema kuwa katika kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari washiriki kutoka nchi 52 za Afrika walitua nchini kwa ajili ya kuhudhuria maadhimisho hayo.

# ACT yaja na hatua tatu kuwakabili 'panya road'

**Na Romana Mallya**

VIKUNDI vya kihalifu mitaani, maarufu panya road, vimekiibuka Chama cha ACT-Wazalendo, kikilitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua tatu kukabiliana nao ikiwamo msako wa kuwabaini.

Hivi karibuni kumeibuka na vikundi hivyo vya kihalifu mkoani Dar es Salaam, vijana hao wakiwavamia usiku wananchi na kuwajeruhi na kupora mali zao.

Kutokana na vitendo hivyo, Msemaji wa Kisekta Wizara ya Mambo ya Ndani wa ACT-Wazalendo, Mbarala Maharagande, kupitia taarifa yake aliyoitoa jana kwa vyombo vya habari, alilitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua za haraka.

Hatua nyingine ambazo chama hicho kimelitaka Jeshi la Polisi kuzichukua ni pamoja na kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili vitekeleze kazi na wajibu wake kwa ufanisi.

"Jeshi la Polisi liwe na operesheni maalumu ya kudhibiti vitendo hivi vinavyohatarisha amani ya wananchi na mali zao kwa kutumia njia za kiusalama kubaini mitandao hii ya kihalifu," alisema.

Maharagande alisema matukio ya wahalifu hao yameripotiwa kwa nyakati tofauti na wakazi wa maeneo ya wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni.

"Vitendo hivi vimedaiwa kufanywa na vijana wanaoitwa 'panya road', mpaka sasa waathirika wakuu wa matukio hayo ni wakazi wa kata za Chanika, Zingiziwa na Mtaa wa Mtongani, Kata ya Kunduchi. Vijana hao wamekuwa na desturi ya kuvamia nyumba moja baada ya nyingine wanaiba, wanajeruhi na kubaka," alisema.

Aliongeza kuwa matukio hayo yamekuwa yakifanyika kati ya majira ya saa nne hadi saa tano mpaka sasa zaidi ya watu 89, wamejeruhiwa kwa mtindo wa kuingia nyumba moja baada ya nyingine.

Alisema wahalifu hao inasemekana wanafanya shughuli zao kwa uhuru mkubwa na huwa inawachukua hadi saa mbili kufanya vitendo vyao huku vituo vikubwa vya polisi vikiwa karibu na maeneo ya matukio.

"Juzi walivamia nyumba ya Mtaa wa Gogo jirani na kituo cha polisi na walifanya vitendo vya kinyama na kuondoka salama. Usiku wa juzi pia walijeruhi watu 19 wa Kata ya Kunduchi," alisema.

Maharagande alisema ACT-Wazalendo inalaani vikali vitendo hivyo vinavyofanywa na makundi ya vijana wahuni na kulitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua stahiki za kulinda raia na mali zao.

**USULI NA HISTORIA**

Katikati ya miaka ya 1990, kuliibuka kundi lililoitwa 'Washawasha' lililoundwa na vijana waliojihusisha na ukabaji, uporaji na ubakaji maeneo ya Kinondoni.

Mwaka 1994, kuliibuka kundi la vijana walioitwa 'Mbwa Mwitu', wakikaba na kupora maeneo ya Mbagala, Tabata na Kigogo mkoani Dar es Salaam.

Kamanda Suleiman Kova aliendesha msako maalum uliofanikisha kunaswa kwa viongozi wao na kudhibiti vitendo hivyo vya kinyama dhidi ya wananchi.

Vilevile, mwaka 1992 kulikuwa na kundi lililoitwa Komondoo Yosso, lililojihusisha na vitendo hivyo maeneo ya Mburahati, Manzese, Mabibo, Kigogo na Kinondoni.

Miaka ya 1990 kulikuwa na kundi lililoitwa 'NATO Mob' lililofanya vitendo vya uhalifu maeneo ya Magomeni na Buguruni, wakivuta bangi hadharani na kutenda unyama huo.

Mbali na Mkoa wa Dar es Salaam, vikundi vya vijana hao viliripotiwa katika Jiji la Tanga mwaka jana, wakijiita 'Watoto wa Ibilisi'.

Mkoani Mtwara mwaka 2014 liliibuka kundi lililoitwa 'Tukale Wapi', nalo likifanya vitendo hivyo dhidi ya wananchi.

Juzi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliitisha kikao na makanda wa polisi mkoani humo kupanga mikakati ya kukomesha unyama huo dhidi ya wananchi.



Wadau mbalimbali wa sekta ya habari, mabalozi pamoja waandishi wa habari wakimsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), alipokuwa akitoa hotuba yake katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Hoja nne kuteka mjadala Wizara Mambo ya Ndani

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO wa Bunge la Bajeti unatarajiwa kuendelea kesho bungeni jijini Dodoma baada ya kusimama kwa siku tano kupisha mapumziko ya mwishoni mwa wiki na sikukuu ya Eid El Fitri.

Ratiba ya mkutano huo ulioanza Aprili 5, mwaka huu, inaonyesha kuwa kesho kutakuwa na mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Katika mjadala huo hoja nne zinatarajiwa kuibuka ikiwamo ya uhaba wa askari polisi na magereza na watumishi wengine wanaosimamia idara na taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo. Tayari Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ameshaweka wazi kuwapo kwa dosari hiyo.

Hoja nyingine inayotarajiwa kuibuka wakati wa mjadala huo ni ukimya uliotanda kuhusu ripoti ya kamati maalum iliyoundwa kufuatilia mauaji yaliyotokea Tanga na Mtwara mwanzoni mwa mwaka yakihusisha askari polisi.

Tayari Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alishakabidhiwa ripoti ya kamati hiyo, naye kutangaza kuiwasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua zaidi.

Kama ilivyokuwa kwenye mikutano mitatu iliyopita ya Bunge la Bajeti, safari hii hoja ya kuwapo msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu kwenye magereza mbalimbali nchini inatarajiwa kuwa sehemu ya hoja muhimu zitakazowasilisha na wabunge wakati wa mjadala wa kesho.

Ripoti ya CAG kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka huu, inabainisha kuwapo msongamano mkubwa kwenye magereza mbalimbali nchini, akitolea mfano Gereza la Keko ambalo limezidisha idadi kwa asilimia 194. Uhaba wa nyumba za askari polisi, magereza na uchakavu wa miundombinu iliyoko ya maeneo hayo, pia unatarajiwa kuwa sehemu ya hoja za mjadala huo.

Ripoti mpya ya CAG inabainisha hali mbaya ya miundombinu ya makazi ya askari magereza, ikiwamo kuharibika kwa mifumo ya maji.

# TEF, MISA zaeleza mazingira vyombo vya habari nchini

**Allan Isack na Idda Mushi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, amesema waandishi wa habari wamekuwa wakikumbana na matatizo mbalimbali ikiwamo kupigwa, kufunguliwa kesi za uongo na kuawa.

Alisema siku ya maadhimisho hayo ya uhuru wa vyombo vya habari, huwa waandishi wa habari wanakumbushana majukumu kati yao na vyombo vya dola kwa maslahi ya nchi.

Alisema washiriki wa madhimisho ya siku hiyo kwa mwaka huu iliyofanyika jana Arusha kwa nchi za Afrika wametoka katika nchi 54 za bara la Afrika.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ya mwaka 2021, jumla ya waandishi 55 waliuawa duniani.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-TANZANIA) na Mjumbe wa Bodi ya MISA KANDA, Salome Kitomari, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ya kuwatumikia Watanzania na aliahidi ushirikiano katika ujenzi wa taifa.

Alisema tangu kuingia madarakani kwa Rais Samia, kumekuwapo na mabadiliko chanya ya ukuaji wa sekta ya habari nchini, ikiwamo uhuru wa kujieleza, upatikanaji wa taarifa na vyombo vya habari vinazidi kuongezeka na kufunguliwa vilivyokuwa vimefungiwa.

"Tunakushukuru wewe na serikali yako kwa kuona tatizo la sheria zinazosimamia taaluma yetu na kuanza kuchukua hatua mbalimbali, ikiwamo mabadiliko ya kanuni ambayo yalikwaza kazi yetu. Lakini jitihada zilizoko sasa za kutushirikisha wadau wote wa habari kupitia sheria za habari, ili kuondoa vifungu vinavyokwaza pande zote ni hatua za kutia moyo," alisema Salome.

Alisema malengo ya kuwapo kwa MISA ni kuhakikisha uhuru wa vyombo vya habari na upatikanaji wa taarifa unakuwapo, ukuaji wa vyombo vya habari imara vinavyowajibika na mazingira mazuri ya uandishi wa habari katika nchi wanachama kwa maendeleo na ustawi wa nchi hizo.

Hata hivyo, alisema sekta ya habari, inakabiliwa na matatizo kutokana na baadhi ya sheria kuwa kitanzi kwa vyombo vya habari, hali duni ya maisha kwa waandishi wa habari kutokana na vyombo vingi kushindwa kulipa mishahara kwa wakati au kutolipa kabisa, kwa sababu mbalimbali ikiwamo hali ngumu ya biashara.

Matatizo mengine ni ushindani usio sawa kwenye matangazo kwa vyombo vya masafa ya ndani na vile vya nje, unaochangia kupunguza mapato kwa vyombo vya ndani ambavyo vimeajiri wengi, ukuaji wa teknolojia ulioleta ongezeko la vyombo vya habari na wananchi kutumia uhuru wao kujieleza mitandaoni.

## ‘Watumishi watapata mishahara mipya Julai’

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema ofisi yake imejipanga kupandisha mishahara ya watumishi wa umma kwa wakati kama alivyoelekeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani 2022 yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma.

Akizungumzia utekelezaji wa maelekezo ya kuwapandisha mishahara watumishi wa umma, Jenista alisema jana kuwa ofisi yake itafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha ifikapo Julai, 2022 kila mtumishi wa umma anapata mshahara mpya. Hivyo amewataka watumishi wa umma kuwa watulivu wakati zoezi hili likiendelea kushughulikiwa na serikali.

“Mimi na watendaji wangu tumeanza kupitia taarifa za watumishi katika Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara ili kushirikiana na Wizara ya Fedha katika kukamilisha zoezi la kupandisha mishahara ya watumishi wa umma itakapofika Julai 2022 kila mtumishi atakuwa amepata mshahara mpya kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais,” Jenista alisisitiza.

Waziri huyo aliongeza kuwa ahadi ambazo Rais amekuwa akizitoa kwa watumishi wa umma zimekuwa zikitekelezwa kwa wakati, hivyo jambo hili la mishahara litatekelezwa kama alivyokusudia.

Katika kuhakikisha mishahara ya watumishi wa umma inapanda kwa mujibu wa maelekezo ya Rais, Waziri Jenista aliwataka maofisa utumishi wote katika taasisi za umma nchini kuhakikisha wanatekeleza ipasavyo kila mwongozo utakaotolewa na ofisi yake kwa lengo la kukamilisha upandishaji wa mishahara ya watumishi.

“Maofisa utumishi hakikisheni mnatekeleza maelekezo yatakayotolewa na ofisi yangu kwa uzalendo na uadilifu wa hali ya juu kwani atakayekwenda kinyume, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kwa kukiuka maelekezo halali ya Mheshimiwa Rais,” aliagiza.

Akizungumzia utekelezaji wa maelekezo mengine aliyoyatoa Rais likiwamo la watumishi waliondolewa kutokana na vyeti vya kughushi, Waziri Jenista alisema wameshafanya mawasiliano na mifuko ya hifadhi ya jamii kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ili jambo hilo nalo lifanyiwe kazi ndani ya muda mfupi kwa mujibu wa maelekezo ya Rais.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Erasto Mhina, akizungumza na wafanyakazi wakati wa sherehe za Mei Mosi 2022, katika uwanja wa mpira wa Jitegemee. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Rais ataka Waislamu, Wakristo kutenda mema baada ya kufunga

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka waumini wa dini za Kiislamu na Kikristo ambao katika kipindi cha miezi miwili kwa nyakati tofauti walifunga Ramadhani na Kwaresma, kuendeleza mafunzo waliyopata ili kuleta amani na utulivu nchini.

Pia amewataka kuendeleza matendo mema waliyokuwa wakiyafanya wakati wa kufunga kwa kuwa mambo mazuri ni ya wakati wote na si kwa kipindi fulani tu.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika Baraza la Eid El Fitr lililofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kiserikali, kisiasa na taasisi tofauti.

Rais Samia alisema Baraza la Eid ni sehemu ya sherehe za kumalizika kwa mwezi Mtukufu unaotoa mafunzo mengi kwa Waislam na madhehebu mengine.

Alisema kama alivyosema Sheikh (Nuru Jabir) Mruma (Katibu Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania- BAKWATA) kwamba mwaka huu wameongozwa na miezi mitukufu kwa kuanza na Kwaresma kwa Wakristo kwa siku 40 na baadaye Ramadhan. “Vipindi vyote viwili vilikuwa ni vipindi vya mafunzo na kumcha Mungu kwa dini zote Wakristo na Waislam. Ni imani yangu kwamba mafunzo tuliyoyapata kipindi hicho kwa pande zote mbili tutaendelea nayo. “Tutaendelea nayo na kufanya Watanzania waumini wa dini mbalimbali tuendelee kuishi maisha ya kumcha Mungu ambayo ndiyo yanayoleta amani na utulivu ndani ya nchi yetu,” alisema.

Rais Samia alisema walishirikiana vyema kwa kufunga na wale ambao hawakufunga waliacha biashara ambazo walijua hazikuwa sahihi.

Alisema kama matendo hayo hayakuwa sahihi wakati wa mfungo hata wakati wa sasa (baada ya kumaliza mfungo) ni sahihi.

Kadhalika aliwataka Watanzania waendelee na ushirikiano na wasikubali kuchezewa na kufarakanishwa kwa misingi ya kidini au kikabila ili wasihatarishe umoja na mshikamano.

“Tujitahidi kuishi kwa kushikamana na kushirikiana katika raha na shida. Hapana faida yoyote ya kufarakana katika kugawana kwa misingi ya kidini. Tofauti zetu za kimaumbile ya mwanadamu, zisitufanye tuvurugane.

“Niungane na Sheikh Nuhu Jabir Mruma kutoa wito kwa Watanzania kutunza na kudumisha usalama na utulivu wa nchi,” alisisitiza.

**AHIMIZA MAADILI**

Kuhusu mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii, Rais Samia alisema kwamba upo ulezi mkubwa ndani ya nchi hasa kwa vijana wa kike na wakiume.

“Namna tunavyosifia maendeleo, namna tunavyofungua nchi, tamaduni za kigeni zinakuja nami niombe pamoja na ombi lenu kwamba somo la dini lifundishwe shuleni, watu wa serikali tupo hapa tutalichukua na kuliangalia.

“Lakini niombe pia kwamba kama wazazi, walezi tukae kwenye msingi ya kidini, kimila na tamaduni zetu katika kulea watoto. Tumejisahau kidogo dunia iko mbele wazazi tuko nyuma. Hawa panya road tunaozungumza leo ni watoto wetu, tumewazaa majumbani mwetu wana dini zao lakini hawakukuzwa kwenye misingi ya kidini. Hili ni kundi moja lakini yako mengine ambayo ni fedheha kuyasema,” alisema.

Kutokana na kukithiri kwa mmomonyoko wa maadili, aliwataka wazazi wa dini zote warudi kwenye misingi ya kidini, mila na desturi kwa sababu kuna mmomonyoko wa maadili.

**CHANJO YA UVIKO-19**

Kuhusu chanjo ya UVIKO- 19, Rais Samia alisema serikali imechanja watu 3,950,839 sawa na asilimia 13 ya kundi walilokusudia kulichanja hiyo inaonyesha Tanzania iko mbele ikilinganishwa na wale waliotangulia kutoa chanjo.

Hata hivyo, alisema ili kufikia lengo lililokusudiwa, kampeni kubwa kwa ajili ya uhamasishaji wananchi kujitokeza kuchanjwa inatarajia kufanyika.

Kadhalika alisema kwa sasa iko ahueni ya maradhi hayo lakini akawaomba Wtanzania wasijiachie bali wachukue tahadhari kwa sababu hawajui kirusi kipya kitaibuka lini au kilichopo kinaisha lini.

Akizungumzia ufunguzi wa msikiti wa Mohamed VI, alisema serikali inalishughulikia suala hilo na kwamba masharti yote ya kiitifaki na kidiplomasia yanakwenda kufuatwa na utaendeshwa kwa misingi hiyo.

**KAULI YA BAKWATA**

Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeir, aliwahimiza Waislamu na Watanzania wamuunge mkono Rais Samia kwa sababu ndivyo wastaarabu na waungwana wanavyofanya.

Awali, Sheikh Mruma aliipongeza serikali kwa kuhakikisha amani na utulivu inaendelea kuwapo na kuwaomba Waislam wailinde tunu hiyo na kushirikiana na wote wanaoilinda.

Sheikh Mruma alisema bado hali ya maadili hairidhishi kwa sababu bado wanaendelea kusikia matendo kama ubakaji wa watoto wadogo na wanawake, mauaji ya watoto kuua wazazi na ukatili.

“Matendo hayo yanaashiria kama jamii tumeacha kumwabudu Mungu kwa haki na badala yake tumetawaliwa na tamaa za mali, tumejitahidi kuelimisha jamii kuhusu kufuata amri na kumfuata Mungu katika misikiti, madrasa lakini hali bado hairidhishi,” alisema.

Aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kurasimisha somo la dini ya Kiislam katika shule ili walimu wa dini waajiriwe na serikali kusaidia watoto wafundishwe misingi bora ya imani na uadilifu kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu.

Pia kwa niaba ya BAKWATA, alimpongeza Rais Samia kwa kuanzisha demokrasia na uzalendo na kukutana na vyama vya siasa na kuunda kikosi kazi kinachoendelea kupokea maoni kwa makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini.

Pongezi zingine zilielekezwa kwa Rais kwa hatua yake ya kutembelea nchi mbalimbali ikiwamo kuzindua filamu ya The Royal Tour ambayo itachochea utalii na kuimarisha uchumi wa nchi.

Pia BAKWATA imetoa wito kwa Waislam kutoa ushirikiano wakati wa sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwezi Agosti mwaka huu na imewataka wale ambao hawajachanja chanjo ya UVIKO-19 wajitokeze kuchanja.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema wana Rais mchakapazi na anayejali wananchi wake ambaye asubuhi (jana) ameswali, ameenda Arusha na kurudi Dar es Salaam na juzi alirudi jioni.

“Panya road na panya buku kuanzia jana wameingia shimoni mkoa wa Dar es Salam wako kimya. Tutasherehekea salama tutakuwa na ulinzi endelevu na hatutakuwa na panya road wala panya buku,” alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Nani anawapa jeuri hawa 'panya road'*

**KUNA** swali moja ambalo linahitaji majibu. Swali hilo ni nani hasa anawapa jeuri kundi la kihalifu maarufu kwa jina la 'panya road' ambalo kwa miaka kadhaa limekuwa likifanya matukio ya kihalifu mkoani Dar es Salaam.

Vitendo hivyo ni kuvamia watu mitaani, kwenye maduka na nyumbani kisha kuwajeruhi kwa kutumia mapanga na kuwapora mali mbalimbali, zikiwamo fedha.

Tumeliuliza swali hili ili yapatikane majibu yasiyoacha shaka yoyote kuhusu kundi hili la wahalifu linapewa jeuri na kulindwa na nani kwa miaka yote.

Kuna mambo kadhaa yanatushangaza yakiwamo umri mdogo wa vijana wanaounda kundi hilo la kihalifu ambao inaelezwa kuwa ni kuanzia miaka 15 hadi 25. Kwamba inakuwaje wanafanya matukio haya bila kujulikana wakati wengi wao wanaishi na wazazi wao?

La pili, je, mamlaka mbalimbali kama za mashina, mitaa na kata haziwafahamu wala familia wanazotoka. Tatu, je, inakuwaje vyombo vya dola hususan Jeshi la Polisi kutowafuatilia na kuharibu mtandao wao kwa miaka yote ambayo wamekuwa wakihatarisha maisha ya wananchi na mali zao?

Haya yote yanatufanya tubaki na swali hilo tulililoiuliza awali kwamba ni nani hasa anawalinda na kuwapa jeuri 'panya road', ambao wamedhihirisha kwamba hawaogopi chochote wala mamlaka yoyote licha ya maonyo ambayo yamekuwa yakitolewa na vyombo vya dola na viongozi wa serikali.

Kikundi hiki kimeibuka upya hivi karibuni na kufanya vitendo hivyo katika maeneo ya Chanika, Tabata kabla ya kutenda unyama Kunduchi siku moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan Jumapili kutoa onyo dhidi ya vitendo vya kihalifu na kulitaja moja kwa moja kundi la 'panya road'. Jumatatu wiki hii majira ya jioni vijana hao walidaiwa kuwakata mapanga watu 19 na kupora mali mtaa wa Mtongani Kata ya Kunduchi mkoani Dar es Salaam, huku Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam likithibitisha kuwakamata sita kati yao.

Tukio hilo ni la pili katika mkoa huo baada ya wiki moja iliyopita katika Wilaya ya Ilala kundi linalodaiwa kuwa la 'panya road' kuvamia nyumba 23, kujeruhi na kuiba mali na fedha.

Mfululizo wa vitendo vinavyofanywa na kundi hilo ni dalili za tishio kubwa la usalama wa maisha ya wananchi na mali zao, kiasi kwamba Rais Samia ameliona hilo na kulitolea kauli.

Rais Samia akizungumza na wafanyakazi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani jijini Dodoma Jumapili, alikemea vitendo vya uhalifu na kuwataka wahusika, wakiwamo 'panya road' kuacha mara moja.

Tukio la Kunduchi lichukuliwe kama changamoto kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuchukua hatua sasa kuhakikisha kwamba kundi hilo linatokomezwa kabisa, kwa kuwa limeonyesha jeuri hata kwa mkuu wa nchi aliyetoa onyo siku moja kabla.

Vyombo hivyo hususan Jeshi la Polisi halinabudi kuweka utaratibu endelevu kuhakikisha kwamba vitendo vyote vinavyofanywa na vijana hao vinadhibitiwa kabla, ikiwamo kuwashirikisha viongozi wote wa serikali kuanzia ngazi za mitaa na jamii nzima kupitia ulinzi shirikishi.

Tatizo tunaloliona ni kwamba yanapotokea matukio la uhalifu, Jeshi la Polisi na wanasiasa wanatoa ahadi za haraka za kuyakomesha, lakini hatua hizo haziwi endelevu, hivyo kujirudia baada ya muda si mrefu.

Juzi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliitisha kikao cha dharura cha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo na kusema wataanzisha operesheni endelevu ya kupambana rasmi na vikundi vya vijana wahuni.

Alisema hawawezi kuwaacha vijana hao wakitamba na bisibisi na mapanga na kutia hofu kwenye jamii, na kwamba kuanzia siku hiyo hakuna atakayesalimika.

Tunaunga mkono tamko la Makalla, lakini ahakikishe operesheni dhidi ya uhalifu inakuwa endelevu. Tunaamini hatua hizi zikichukuliwa, jibu la swali nani anawapa jeuri 'panya road' litapatikana sambamba na kuufuta kabisa mtandao huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# *Viongozi na waandishi Afrika wachukue hatua*

Na Mwandishi Wetu

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, anahitimisha kilele cha Siku ya Uhuru wa Habari Duniani kwa Afrika, akiwaonya waandishi wa Afrika, kujitazama kwani wanairipoti vibaya Afrika kama vile ambavyo wanahabari wa kigeni wanavyoendeleza taarifa mbaya kuhusu bara hilo.

Anapowahutubia waandishi wa Afrika jijini Arusha jana, Rais anasema ni kama vyombo vya habari vya Afrika vinavisaidia vile vya kigeni kuendelea kuichafua Afrika, jambo ambalo anasema si jema kwa bara hilo.

Anapowageukia wanahabari wa Tanzania anasema kuna mengi mazuri ya kuripoti lakini kila wakati yanasahaulika na uandishi unakuwa wa matukio mabaya zaidi yanayodhalilisha badala ya kuleta matumaini na mwangaza wa maisha ya wasomaji na jamii inayoandikwa.

Anatoa mfano kuwa imekuwa ni kawaida watu kuimba wimbo wa umaskini miongoni mwa Waafrika kuwa wanaishi chini ya Dola moja kwa siku ambayo ni takribani shilingi 2,300.

Rais anasema nadharia hiyo hajaikubali na mara nyingi anaipinga wakati akikutana na wanaoitetea, akiwafahamisha kuwa wapo watu wanaoishi kwa kula matunda mbalimbali tena yanayozalishwa kwa kilimo kisichotumia kemikali, mbolea na viuatilifu vya viwanda, chakula ambacho kinauzwa ghali kwenye 'supa maketi' za Ulaya na Marekani, hivyo siyo kweli kuwa watu wanaishi chini ya Dola moja.

Anatoa mfano wa wafugaji kama Wamasai wanaoishi kwenye nyumba za asili ambao wana utajiri mkubwa wa mifugo ambayo pekee inadhihirisha kuwa si maskini kama inavyoelezwa.

Anawaambia wanahabari kuwa wabadilike na kuanza kuandika mengi mazuri ya Afrika na Tanzania na kulipenda bara lao. Kwa hivyo anawahamasisha kujikita katika kuikabili dhana potofu kuhusu bara la Afrika na kukuza uandishi na utangazaji wa ripoti zenye uwiano na uhakika.

Ni vyema angalizo za Rais likafanyiwa kazi kuhusu kuripoti mabaya kuhusu Tanzania na hata Afrika. Ni kweli kuwa taarifa nyingi zikitafitiwa zinaonyesha upungufu zaidi. Kwa mfano miaka ya nyuma habari za wanawake kwenye vyombo vya habari vingi zilihusu udhalilishaji kama ubakaji, mimba, jinai na kwa ujumla taarifa mbaya wakati mwingine zikiambatana na picha za waathirika hao.

Hata hivyo, juhudi zilifanyika na kubadilisha sura hiyo na sasa ripoti za masuala ya kinamama zinawaonyesha wakiwa na mafanikio badala ya kubakia kuwa wadhalilishwaji.

Pamoja na nia njema ya Rais kuwahimiza wanahabari kuandika masuala ya maendeleo na mafanikio ukweli ni kwamba viongozi wa Afrika wanawajibu wa kuimarisha sekta ya habari ya umma, ili kuwa na mashirika ya habari ya umma, redio na televisheni za umma badala ya uandishi wa Afrika kutegemea kupata habari za Kiafrika kupitia mashirika ya kigeni ambayo nayo huiandika vibaya Afrika.

Ni wazi kuwa vyombo vya habari vya Afrika vinategemea habari za Afrika kutoka mashirika ya Reuters, au BBC yote ya Uingereza, AFP la Ufaransa, Xhnua la China ili kupata taarifa za nchi za Kiafrika.

Pengine kama kungekuwa na vyombo vya habari vya Afrika vyenye taarifa sahihi na zinazoelezea mema ya Afrika utegemezi wa mashiriki au vyombo vya kigeni ungepunguzwa.

Rais na viongozi wa Afrika wanapaswa kuelewa kuwa baadhi ya vyombo vya habari havina fedha hivyo kutegemea vyanzo vya nje, vikiwamo mashirika makubwa ya habari ili viendelee kuwepo hivyo ni lazima serikali zisaidie vyombo hivyo kwa kuvipa matangazo, kuweka mazingira wezeshi, kuondoa sheria mbovu na kandamizi ili kuviwezesha kufanikisha lengo la uandishi unaoleta mabadiliko na maendeleo badala ya ule wa kulalamika na kutangaza ubaya wa serikali zao.

HABARI KITAIFA

## Polisi waendelea kuchunguzwa kwa tuhuma za rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, imeendelea na uchunguzi wa askari polisi wanne ambao wanatuhumiwa kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa huo, Leonidas Felix, alisema askari polisi hao wanatoka wilaya mbalimbali za mkoa wa Geita, na kwamba uchunguzi ukikamilika watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Felix alisema katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka 2022, TAKUKURU Mkoa wa Geita imefanya kazi ya uzuiaji wa vitendo vya rushwa kwa kiziba mianya inayochangia uwapo wake kwa kuendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma.

Aidha, alisema jumla ya miradi ya maendeleo 19 katika sekta za afya, elimu, ujenzi, maji na kilimo yenye thamani ya Sh. bilioni 18.67 ilifuatiliwa. Thamani hiyo ni kwa mujibu wa mikataba ya miradi husika.

Alisema miradi 15 yenye thamani ya Sh. bilioni 18.3 ilibainika kuwa na mapungufu ya kutozingatiwa kwa vigezo na masharti yaliyoainishwa kwenye michoro na kukosekana kwa usimamizi thabiti kutoka kwa wataalamu wa halmashauri, pamoja na baadhi ya mafundi walioshinda zabuni za ujenzi kutokuonekana katika eneo la mradi na kuwaacha mafundi wasaidizi pasipo usimamizi wala maendeleo eneo la ujenzi. Baada ya ufuatiliaji huo, wahusika walishauriwa namna bora ya kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo kupitia vikao kazi.

"Katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka 2022, tumepokea taarifa za malalamiko 75 ambapo taarifa zilizohusu rushwa ni 40 na 35 hazihusiani na rushwa, hivyo tumezitolea ushauri na kuelekeza walalamikaji mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao. Sekta inayoongoza kwa malalamiko ni eneo la Serikali za Mitaa 32, binafsi 10, fedha 7, elimu 8, misitu 3, sekta ya madini 3, afya 3, ardhi 3, polisi 2, mahakama 1, ujenzi 1 na zilizohusu siasa 2," alisema.

# Mbaroni kwa tuhuma za mauaji ya mwalimu, wizi

**Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watuhumiwa 20 kwa makosa mbalimbali yakiwamo ya mauaji ya mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bwiru na wizi wa televisheni.

Kadhalika, Idara ya Uhamiaji mkoani Mwanza, inawashikilia raia 68 wa Ethiopia kwa kuingia nchini kinyume cha sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alisema kuwa watu hao 20 wakiwamo walinzi wa ghala lililokuwa na televisheni hizo walitengeneza funguo za bandia na kuzitumia kufungua na kuiba.

"Tunawashikilia jumla ya watu 20 ambao wanatuhumiwa kwa kuiba televisheni 160 mali ya kampuni ya ZAK inayomilikiwa na raia kutoka China, wezi hao kwa kushirikiana na walinzi wa kampuni hiyo ambao walitengeneza funguo za bandia na kuiba televisheni hizo," alisema Kamanda Ng'anzi.

Aidha, kamanda alisema watu watano wanashikiliwa kwa tuhuma za kuvamia nyumba ya mwalimu huyo.

Katika tukio hilo watu hao wanadaiwa kumuua mwalimu huyo kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali kilichomsababishia umauti na kuiba vitu vyake vya ndani ikiwamo televisheni, pasi ya umeme, redio na mtungi wa gesi.

Katika hatua nyingine Idara ya Uhamiaji mkoani Mwanza inawashikilia wahamiaji haramu 68 kutoka Ethiopia kwa kuingia nchini bila kibali.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza, Peter Mbaku, alithibitisha kukamatwa kwa wahamiaji waliokamatwa Aprili 29 katika kijiji cha Sanjo Kata ya Usagara Wilaya ya Misungwi mkoani humo.

Mbaku alisema walikamatwa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi baada ya kupata taarifa za kiintelijensia.




Ofisa Uhusiano wa Benki ya CRDB, Tawi la Palm Beach, jijini Dar es Salaam, Theresia Mwamunyange (kulia), akikabidhi fedha Sh. milioni 10 kwa mshindi wa droo kubwa ya Mei Mosi ya Bahati Nasibu ya Biko, Muhidin Salumu Hassan, jijini humo mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Balozi wa Biko, Kajala Masanja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kutunza miti ili kuzuia tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MKUU wa Wilaya ya Mkoani, Khatib Juma Mjaja, amesema ukataji wa miti kiholela ndani ya wilaya yake haukubaliki na endapo atakamatwa mtu ambaye amekata mti bila kupata kibali husika, atachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema, suala hilo halitokuwa na msamaha kwa mtu yoyote ambaye atabainika, kwani vitendo hivyo vinasababisha eneo hilo kuwa na jangwa hali inayochochea athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mjaja aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na mwandishi wa habari hizi ofisini kwake Mkoani, ambapo aliitaka jamii kuendelea na utaratibu wa upandaji wa mikoko ili kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema, Mkoani ni miongoni mwa wilaya ambazo zipo kando kando mwa bahari, hivyo zinaweza kutokea athari zozote, kwani wilaya hiyo imezungukwa na visiwa vidogo vidogo sita.

"Mabadiliko ya tabia nchi ni kauli mbiu ya dunia kwani athari zake zimekuwa zikileta majanga mengi duniani, wilaya yetu ni miongoni mwa waathirika wa mabadiliko haya," alisema.

Alieleza, kuna jitihada mbalimbali ambazo serikali imekuwa ikizichukuwa katika kukabilikana na mabadiliko hayo ikiwamo kisiwa kidogo cha Makoongwe ambapo baadhi ya maeneo yalishawahi kujitokeza athari katika miaka ya nyuma.

Alisema, kwa upande wa Kisiwa Panza serikali ina maeneo ambayo imejenga kuta za kuzuia maji yasiingie kwenye makazi ya watu ambapo mradi huo umetekelezwa kupitia ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Mjaja alieleza kuwa, wamejipanga kutoa elimu kwa jamii, katika kipindi hichi cha kuanza kwa mvua za masika ili waweze kujikinga na athari zinazoweza kutokea.

"Tumeanza kufanya ziara maeneo hatarishi ambayo yalishatokea athari za mabadiliko ya tabia nchi katika eneo la Mbuyuni, ambalo yalijitokeza maporomoko, eneo ambalo maji yanaingia na kuathiri ardhi Makombeni na Chole Kengeja ambako maji mengi yanatuama kipindi cha mvua," alisema.

Alifahamisha kuwa, wakazi walipotembelea maeneo hayo waliwashauri wananchi ambao wanaishi kwenye maeneo hayo, jinsi ya kuchukua juhudi mbalimbali za kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema, vile vile yapo matuta ambayo yamejengwa kwa ajili ya kudhibiti maji ya bahari yasipande juu katika eneo la Chole Kengeja.

Aliongeza kuwa kila mmoja anawajibu wa kutunza mazingira, kwani athari ya mabadiliko ya tabia nchi yanapotokea huathiri hadi kilimo.

# Serikali kuunga mkono SUA utafiti kuinua maendeleo

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, imeahidi kuunga mkono juhudi za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kutokana na kufanya utafiti unaolenga kuinua maendeleo ya Watanzania kwa kufunganisha masuala mbalimbali yanayolenga kuboresha uchumi na kuleta maendeleo kwa taifa.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema hayo juzi mjini hapa wakati akifungua kikao kazi cha wadau wa mradi wa biashara, maendeleo na mazingira iliyohusu uwasilishaji matokeo ya awali ya utafiti wa mradi huo.

Kigahe alisema, mradi huo unatekelezwa katika kipindi muafaka ambacho serikali inasisitiza uwekezaji kupitia sera ya nchi ya kuinua uchumi kupitia uwekezaji katika sekta ya viwanda na biashara.

"Imani yangu kuwa kwa kipindi hiki cha miaka mitano ambayo mradi huu utatekelezwa utasaidia sana kufunganisha shughuli za biashara inayotokana na bidhaa za kilimo, wanyamapori na sekta nyingine," alisema Kigahe.

Naibu Waziri alisema, lengo ni kuhakikisha kuwa biashara ya mazao hayo yanakuwa ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi ambao utakuwa shirikishi kwa ajili ya kupunguza umaskini na kuleta maendeleo endelevu nchini.

Kiongozi wa Mradi wa Biashara Maendeleo na Mazingira nchini, Prof. Reuben Kadigi, alisema dhumuni la kikao kazi hicho ni kuwasilisha matokeo ya awali ya utafiti wa mradi huo wa kile ambacho kimeshapatikana kwa muda mfupi kwa utafiti wa awali.

Prof. Kadigi alisema, mradi huo ni wa miaka mitano, umeanza mwaka 2019 na utakamilika Machi, 2024 na unatekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na washirika kutoka nchi 15 tofauti za Afrika, Asia, Uingereza na Brazil.

Prof. Kadigi alisema, lengo la mradi huo ni kuhakikisha biashara ya mazao ya kilimo na wanyamapori inakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi shirikishi ili kupunguza umaskini.

Alisema moja ya njia ya utekelezaji wa Maendeleo Endelevu ni kutoharibu mazingira na upotevu wa viumbe hai hususani katika sekta ndogo za sukari, soya, kahawa, nyamapori na wanyamapori.

"Kazi yetu kwenye mradi ni kushughulikia changamoto ngumu na jinsi ya kuondoa athari mbaya kwa jamii na mazingira zinazosababishwa na biashara ili tufanye biashara ambayo itatusaidia kutuendeleza kuleta maendeleo, lakini kuzingatia madhara kwenye uhalisia wa mazingira," alisema Prof. Kadigi.

Kwa upande wake, Mhadhiri Mwandamizi wa Uchumi, Kilimo na Masoko wa Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA), Dk. Fulgence Mishili, akizungumza kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu hicho alisema, SUA itaendelea kuhakikisha utafiti unafanyika na kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii na taifa.

Dk. Mishili alisema, lengo la kuendelea kufanya utafiti zaidi ni kuiwezesha serikali kufanya uamuzi sahihi kupitia matokeo ya utafiti wa kisayansi katika utekelezaji wake.

Awali, akizungumza kwa niaba ya Rasi wa Ndaki ya Uchumi na Stadi za Biashara Kilimo katika Chuo Kikuu hicho, Dk. Charles Mgeni alisema, SUA itaendelea kushirikiana na serikali kutafuta ufumbuzi na kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili biashara ya bidhaa za kilimo na ya wanyamapori nchini ili kuboresha sera za kibiashara na uchumi na kuleta tija na ufanisi kwa wananchi.



Mkuu wa Dawati la Elimu la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Kinondoni, Bibie Msumi, akizungumza katika uzinduzi wa kampeni ya kupambana na rushwa ya 'Sepesha Rushwa', jijini Dar es Salaam juzi, ambayo inayoendeshwa na asasi ya kiraia ya Ant-corruption Voices Foundation. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mitawi aagiza utekelezaji mradi kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Hassan Mitawi, ameelekeza mradi wa ukarabati wa tuta la kuzuia majichumvi katika Bonde la Ukere, Micheweni Mkoa wa Kusini Pemba, ukamilike haraka ili kuwapa fursa wananchi kuendelea na kilimo cha mpunga.

Alitoa maelekezo hayo jana wakati wa ziara akiambatana na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Thabit Idarous Faina, na watendaji wao katika eneo hilo kwa ajili ya kukagua Mradi wa Urejeshaji Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula (LDFS).

Mitawi aliyemwakilisha Katibu Mkuu, Mary Maganga, alisema kitendo cha ucheleweshaji wa mradi huo kinasababisha wananchi katika maeneo mengine kukosa fursa ya kutekelezewa mradi kama huo. Alionyesha kushangazwa na kuchelewa kuanza kwa ukarabati wakati tayari serikali ilishatoa fedha kupitia mradi huo muda mrefu, ili kusaidia kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika eneo hilo zilizosababisha majichumvi kutoka baharini kuingia kwenye bonde hilo.

"Tutakumbuka eneo hili kabla lilikuwa likitumika kwa kilimo cha mpunga lakini baadaye liliharibiwa na mvua, Ofisi ya Makamu wa Rais ikaombwa kusaidia kutatua changamoto hii kwa kukarabati tuta hili," alisema Mitawi.

Naye Faina alitaka uandaliwe mpango kazi utakaoonyesha shughuli hizo zitakamilika baada ya muda gani.

Faina alisema mpango kazi huo utasaidia kuona nini kinakwamisha mradi ili kupatia ufumbuzi na hatimaye wananchi waendelee na shughuli za kilimo cha mpunga kama awali.

Alimtaka Mratibu wa Mradi wa LDFS katika Wilaya ya Micheweni, Abdallah Hamad Faki, pamoja na watendaji wengine kufunga mikanda ili kukamilika haraka kwa kuwa bonde hilo linatoa ajira kwa wananchi.

Hata hivyo, mratibu huyo alisema kilichokwamisha ni ukosefu wa njia ya kufikisha malighafi katika eneo walilopaswa kujenga tuta.

Mratibu wa Mradi Ofisi ya Makamu wa Rais, Joseph Kihaule, alisema shughuli ya ukarabati wa tuta ulipaswa kuanza tangu Machi 2022 kwasababu tayari fedha zilishapelekwa.

Alisema kimsingi shughuli hiyo ilipaswa kutekelezwa kwa kutumia 'force account' kama ilivyokubalika, ili iende kwa haraka lakini bado inaonekana kucheleweshwa.

# Wanafunzi wapewa jukumu elimu ya rushwa

**Na Sabato Kasika**

WANAFUNZI wametakiwa kuanzisha klabu za kuelimisha madhara ya rushwa shuleni na vyuoni ambazo zitawasaidia kuwa mstari wa mbele kupinga rushwa kuanzia kwenye elimu na hata sehemu ya kazi au biashara.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam juzi na Mkuu wa Dawati la Elimu kutoka Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni, Bibie Msumi.

Msumi alikuwa akizundua kampeni ya kupambana na rushwa iitwayo 'Sepesha Rushwa', ambayo inaendeshwa na asasi ya kiraia ya Ant-corruption Voices Foundation ikihusisha vijana wakiwamo wanafunzi wa vyuo.

"Nendeni mkaanzishe klabu za kupinga rushwa huko vyuoni, ili kila mwanafunzi ajue madhara yake aitae kuanzia shuleni, mitaani, hata maeneo ya kazi anatakapohitimu chuo na kuajiriwa," alisema Msumi.

Aidha, alisema vijana wote kwa ujumla hawana budi kuhimiza jamii kuzuia rushwa, na kwamba kampeni hiyo iwaunganishe ili walete mabadiliko katika jamii lenye lengo la kukataa kila aina ya rushwa.

"Rushwa inashusha maendeleo ya taifa, inashusha uchumi, hivyo wanafunzi na vijana wote kwa ujumla hawana budi kushiriki kikamilifu katika kampeni hii kusaidiana na serikali kuitokomeza," alisema.

Ofisa Uhusiano na Uratibu wa aasisi hiyo, Asumwisye Bambengile, alisema kampeni hiyo ni ya miaka miwili, na kwamba itagusa mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha.

Bambengile alitaja sababu za kuchagua mikoa hiyo kuwa ni Dar es Salaam ni jiji lenye watu wengi na lina mambo mengi pia na kwamba Dodoma ni makao makuu ya nchi na Arusha ni eneo la utalii mkubwa nchini.

"Tutafika katika mikoa hiyo kufanya kampeni, lakini sehemu kubwa ya kampeni yetu itakuwa mtandaoni, ambako mabalozi wa asasi hii wengi wao ni wanafunzi na vijana, watakuwa wanatumia," alisema Bambengile.

Alisema, asasi hiyo imejitosa kusaidiana na serikali katika vita dhidi ya vitendo vya rushwa kuanzia shuleni, vyuoni, kwenye jamii na sehemu ya kazi ili kuwa na jamii ambayo inajali utu kwa kuwa rushwa ni adui wa haki.

Mwenyekiti wa asasi hiyo, Abel Otieno maarufu kama 'MC Reyvan', alisema, jambo la muhimu ili kupambana na rushwa ni kubadili tabia, na kwamba huo ndiyo ujumbe ambao wanaoueneza kwenye jamii kupitia mitandao ya kijamii.

"Hata kaulimbiu yetu inasema, 'Badili Tabia Sepesha Rushwa' hii ina maana kwamba kila mmoja wetu atabadili tabia na kurudi kwenye maadili atakuwa amesaidia kusepesha rushwa," alisema Abel.

## Watakiwa kuandika habari za maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAANDISHI wa habari kisiwani Pemba wametakiwa kuandika habari zinazolenga kuhamasisha maendeleo ya nchi.

Akifungua kongamano la kuelekea maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, lililofanyika katika Ukumbi wa Samael Gombani, Chake Chake, Mratibu wa sekta binafsi Pemba, Ashrak Hamad Ali, alisema nguvu za waandishi ni kubwa katika kuchapuza maendeleo katika nchi.

Alisema kuwa, kuna mambo mbalimbali yatakayosaidia kuwepo maendeleo katika jamii, ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia rasilimali za bahari, kutangaza utamaduni na utalii, kuandika habari za rushwa na udhalilishaji.

“Katika nchi yetu kuna uhuru wa vyombo vya habari, hivyo uhuru huu utusaidie kuchapuza maendeleo na sio kuleta mfarakano, kwa sababu ya nguvu yenu mkiitumia vizuri tutavuna mazuri na mkiitumia vibaya mtasababisha migogoro”, alieleza Mratibu huyo.

Aidha, alivishauri vyanzo vya habari kutoa ushirikiano kwa kuwapa taarifa waandishi pale wanapohitaji, kwa lengo la kuisaidia jamii katika kuwapasha habari.

“Kufuata maadili ni muhimu katika kazi yenu ya habari, kwani kinyume chake mnaweza kuchafua amani iliyoko na kusababisha vurugu na mwisho wake nchi kukosa maendeleo,” alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa Klabu ya Waandishi wa Habari Pemba (PPC), Ali Mbarouk Omar, alisema wanaadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari ili kuhakikisha kuna uhuru wa vyombo vya habari, kuwakumbuka wale wote waliopita ambao walipata madhara pamoja na kuwafahamisha wadau kuwa kuna uhuru wa habari.

“Sauti zetu wanahabari zisaidie wananchi kufanya maamuzi, wafichue maovu, kuhimiza haki, usawa na uwajibikaji, kujenga maridhiano na umoja pamoja na habari zinazojali maslahi ya umma,” alifahamisha mratibu huyo.

Mratibu huyo alieleza kuwa, siku zote habari zinajenga ujasiri wa mtu na ni sauti mbadala kwa wanaoogopa kupaza sauti zao kutokana na hofu, hivyo ni vyema kwa waandishi kuifikia jamii kuibua matatizo yanayowakabili, ili yapatiwe ufumbuzi unaofaa.

Naye Makamu Mwenyekiti wa PPC Khadija Kombo Khamis, alisema, ushirikiano unahitajika kati ya wadau na waandishi wa habari katika kuhakikisha wanasaidia upatikanaji wa taarifa ambazo zitasaidia katika maslahi ya Taifa.

“Pasi na kuwa na vyombo vya habari nchini hakuna chochote kinachoweza kuendelea, hivyo ni muhimu kwa wadau kutoa taarifa na sio kuficha,” alieleza.

Akichangia katika kongamano hilo, Mkurugenzi wa mtandao wa Jamii tv, Ali Massoud Kombo, alisema pamoja na kujitahidi kuibua matatizo kwenye jamii lakini bado wanakabiliwa na tatizo la baadhi ya viongozi kuwaingilia kwenye mamlaka yao, jambo ambalo sio sahihi.

“Baadhi ya viongozi wanatumia mamlaka yao vibaya kwa kutuwekea mipaka na kutupangia habari za kuzitoa wanazozitaka wao, hivyo tunasema wasituingilie katika kazi zetu,” alisema Mkurugenzi huyo.

# Vikwazo vya uwekezaji vyaanza kushughulikiwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeanza kuzifanyia kazi changamoto na vikwazo wanavyopata taasisi na kampuni zinazotaka kuwekeza kwa kuanzisha mchakato wa kutengeneza mfumo mmoja utakaotoa huduma za haraka ikiwamo vibali vya kuwekeza ikiwa njia mojawapo ya kuvutia uwekezaji hapa nchini.

Taasisi hizo ambazo zitaungana kwa ajili ya mfumo wa pamoja wa serikali ni pamoja na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Jeshi la Uhamiaji, Idara ya Kazi, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kikao cha wakuu wa taasisi hizo kilichofanyika mjini hapa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa (BRELA), Godfrey Nyaisa, alisema mfumo huo utaweza kutoa huduma kwa mwekezaji kupitia dirisha la mahala pamoja ili kuondoa vikwazo mbalimbali.

Alisema mfumo huo pia utaweza kupunguza vikwazo kwa wawekezaji nchini ili waweze kuvutiwa kuwekeza kwa ajili ya kuongeza pato la serikali yatayoenda kusaidia kuboresha huduma kwa jamii.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, alisema mfumo huo utamwezesha mwekezaji kukamilishwa taratibu zote kwa muda wa siku moja ama tatu ili aweze kuendelea na utaratibu wake mwingine wa uwekezaji ama kuazisha biashara.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa TIC, John Mnali, alisema mfumo huo utasaidia kutatua changamoto mbalimbali kwa wawekezaji pindi zitakapotokea huku ikiwa njia mojawapo ya kuongeza uwekezaji.

Alisema kuwa licha ya kuwa na dirisha moja ya huduma kwa wawekezaji, lakini wawekezaji kwa sasa wanalazimika kujaza fomu mbalimbali za kuwezesha kusajili, kupata kibali cha kuanzisha biashara ama uwekezaji, kuruhusiwa kufanya kazi.

Kwa upande wake Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Morogoro, Frank Minzikuntwe, alisema mfumo huo utasaidia wawekezaji kupata hati ya ardhi kwa haraka zaidi.



Baadhi ya wanachama wa vikundi vya ujasiriamali vya Kata ya Bonyokwa, jijini Dar es Salaam, wakiwa katika mafunzo ya kuwajengea uwezo utakaowawezesha kuendesha shughuli za ujasiriamali kwa ufanisi, yaliyoendeshwa na wataalamu kutoka kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ‘Watoto wenye ulemavu wafunzwe kujitegemea’

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

OFISA Ustawi wa Jamii, Manispaa ya Morogoro, Rehema Malimi, amevitaka vyama vya watu wenye ulemavu kuwaelimisha wazazi na walezi wenye watoto walio kwenye kundi hilo kuwajengea uwezo wa kujitegemea tangu watoto kwa kufundishwa kufanya shughuli au kazi ndogondogo za nyumbani na kushiriki michezo na watoto wenzao.

Rehema alitoa rai hiyo jana wakati wa mdahalo wa ajira jumuishi ulioshirikisha vyama vya watu wenye ulemavu na asasi za kiraia na kwamba baadhi ya wazazi huanza kuwadumaza watoto wao kwa kutowafundisha kufanya kazi tangu wakiwa wadogo.

Alisema pia endapo wazazi watakuwa na utamaduni wa kufanya watoto wao kuchangamana na wengine na kushiriki katika elimu na michezo, itawafanya kuzoea mazingira hata watakapokuwa wakubwa wataona kuwa na jambo la kawaida kujitegemea na kufanya kazi.

“Watoto wenye ulemavu washirikishwe kwenye kila jambo linalohusu watoto katika maeneo yao, wafundishwe kufua, kuosha vyombo kama ilivyo kwa wengine kama wanacheza mpira nao washiriki, wajengewe urafiki na familia nyingine ili hata baadaye inapotokea kuna fursa wasionekane wa ajabu wala wao wenyewe wasione ni jambo geni kwao,” alisema.

Hassan Mikazi, Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ualbino (TASA), Mkoa wa Morogoro, alisema licha ya serikali kuweka sheria ya kutenga asilimia tatu za kutoa ajira kwa watu wenye ulemavu, bado changamoto ni namna ya wenye ulemavu kuzifikia fursa hizo hasa katika utoaji wa matangazo au taarifa za ajira.

Alisema kama vyama vya wenye ulemavu wameridhishwa na jitihada za serikali katika kusimamia sera hiyo ya ajira jumuishi, lakini changamoto iliyoko ni baadhi ya waajiri kushinda kutekeleza sera hiyo ikianzia wakati wa utoaji taarifa.

“Kweli sera inatekelezwa, lakini shida inakuja kwamba mtoaji wa ajira anatoa taarifa kupitia radio au runinga au hata wengine wanabandika matagazo kwenye nguzo barabarani mara nyingi hawazingatii kama kuna watu wasioona wenye vigezo au wasiosikia ambao wanaweza kupata kazi husika na wakaifanya kwa ufanisi,” alisema.

Naye Athumani Mohamed, Mweka Hazina Chama cha Wasioona (TLB) Morogoro, alisema pamoja na mambo mengine bado vyama vya wenye ulemavu havijawajibika ipasavyo katika kuwaandaa wenye ulemavu kutumia fursa ya ajira iliyoko.

Alisema viongozi wa vyama hivyo wataweka mkazo wa kuwahamasisha wazazi na walezi katika suala la elimu kwa watoto wao bila kuwabagua itakuwa rahisi hata kuzifikia nafasi za ajira zinatolewa.

“Kuna kulegalega kwetu kama vyama viongozi wengi kwenye kuwaandaa wanachama wetu kuzifikia fursa za ajira wengi wa viongozi wanakaa kwa kujali maslahi yao tofauti na walipokuwa wanaomba kura za kuongoza wenye ulemavu,” alisema.

# Wakulima waonywa kwa udanganyifu zao la pamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa pamba katika Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameonywa kuchanganya mafuta ya mnyama kenge kwenye pamba ili kuongeza uzito.

Hatua hiyo inachangia wakulima hao kuuza pamba chafu ambayo haifai katika masoko ya kimataifa.

Aidha, wananchi hao wamekuwa wakichanganya na maji, mchanga pamoja na mawe kwa lengo la kuongeza uzito ili wapate kilo nyingi na kujipatia fedha zaidi katika mauzo ya pamba.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Uyogo katika ziara yake ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hususani sekta ya afya, maji, elimu, kilimo na miundombinu ya barabara.

Alisema wakulima wengi wamekuwa na tabia ya kuchanganya vitu mbalimbali kwenye pamba ili iwe nzito.

Alisema wananchi hao wanachanganya mafuta ya kenge, maji, mawe na mchanga ili kuongeza uzito na kwamba msimu huu kwa mkulima atakayebainika atawajibishwa kisheria.

Pia, alisema msimu huu bei elekezi ya serikali kwa kilo moja ya pamba ni Sh. 1,560 ikilinganishwa na msimu uliopita iliyokuwa Sh. 1,050 na Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), kitainunua kwa bei ya juu, kila mkulima ahakikishe pamba yake inakuwa safi.

Cherehani alisema kila mkulima atapata fedha yake papo hapo baada ya kuuza pamba yake sokoni badala ya kusubiri fedha kama ilivyokuwa katika vipindi vilivyopita na kwa wale wakulima walikopeshwa pembejeo hawatakatwa fedha yoyote kwa sababu serikali inawajali na inataka wazalishe zao hilo zaidi.

Alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 16 za ununuzi wa mbengu za pamba na kuzigawa kwa wakulima nchi nzima na Sh. bilioni 60 kwa ajili ya kununua viwatilifu na kuwataka kulima na kuvuna zao hilo kwa kufuata kanuni bora za uvunaji ili kupata pamba safi.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Masanja Elias alisema, msimu huu ana uhakika wa kupata pamba safi kwa sababu wakati wa kilimo alimshirikisha mtaalamu wa kilimo.




Meneja wa Wateja Binafsi wa Tigo Pesa, Mary Rutta (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 25 kwa Suzanne Daniel, mkazi wa Kigamboni, baada ya kuibuka mshindi wa droo kubwa ya promosheni ya Pesa Mwaa Mwii na Tigo Pesa, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi Mkupuka kunufaika huduma za afya

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

WANANCHI wanaoishi jirani na kikosi cha Jeshi 830 KJ kilichoko Mkupuka, Kata ya Mchukwi, wanatarajia kuanza kunufaika na huduma za afya pamoja na maji baada ya kukamilika kwa ujenzi wa miradi hiyo.

Kaimu Mkuu wa Kikosi 830 KJ, Meja Victor Nkya, alisema zahanati hiyo ambayo imejengwa nje ya eneo la jeshi imekamilika hivi karibuni na inatarajia kuanza kutoa huduma kwa maofisa wa jeshi pamoja na wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Meja Nkya alisema mradi wa maji wa kisima uliojengwa katika zahanati hiyo utaondoa kikwazo cha kukosekana kwa huduma hiyo hususani kwa wanaofika kupata huduma za afya.

Alisema kukamilika kwa kisima hicho pia itawanufaisha wananchi wanaoishi karibu na zahanati pamoja na wanaofika kupata matibabu.

Aidha, alisema Mwenge wa Uhuru wa mwaka huu umepita katika miradi ya kikosi hicho na kuizindua ili iweze kuanza kutoa huduma.

Meja Nkya alisema upo mradi endelevu pia wa shamba la ufuta na korosho uliozinduliwa ambao msingi wake ni kutoa elimu kwa vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wanaopata mafunzo kwa mkataba kwa miaka miwili na wa mujibu wa sheria.

Alisema malengo mengine ni kuendelea kukijengea uwezo kikosi ili baadaye waweze kuwa na mapato yanayoendesha shughuli zao za ndani.

Alisema zahanati hiyo ilikamilika, lakini ilikuwa haina maji na kukamilika kwa mradi wa maji itasaidia zahanati kuanza kutoa huduma.

Mwenge wa Uhuru unaendelea kukimbizwa mkoani Pwani na leo utakuwa katika Wilaya ya Mafia kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo.

# Ukosefu huduma mawasiliano wakosesha mapato

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UKOSEFU wa huduma ya mawasiliano katika Kata ya Bukomela Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga imetajwa kusababisha serikali kuendelea kukosa mapato yake kupitia magulio na minada baada ya mashine za kukusanya mapato kutegemea mtandao na kushindwa kufanyakazi vyema.

Hayo yalibainishwa jana na wananchi wa kata hiyo katika mkutano wa hadhara uliotishwa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani wa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wake jimboni.

Mtendaji wa Kijiji cha Ngokolo, Jenipha Lucas, alisema, wakati magulio na minada kunapofanyika shughuli za kibiashara wanashindwa kukusanya ushuru ipasavyo kwa ukosefu wa huduma ya mtandao na wakati mwingine wanalazimika kuwaruhusu wafanyabiashara kwenda kukatiwa ushuru kata za jirani zenye mtandao.

Alisema, hata utumaji wa taarifa za kiofisi kwenda halmashauri wanalazimika kupanda mlima uliopo umbali wa kilometa moja kutoka kwenye kata kutafuta mtandao au kutembea umbali wa kilometa 12 kwenda Kata ya Nyamilangano, kupeleka taarifa halmashauri na kwenye mtandao wa uhakika.

"Watendaji tunapata madeni ya tozo za serikali wakati wa ukusanyaji wa ushuru kwa wafanyabiashara, tunapoingiza kwenye mashine zaidi ya mara mbili mtandao unapogoma mashine inatuandikia madeni...tunaomba kupata huduma ya mtandao wa uhakika ili kutoa zero hii," alisema Lucas.

Paskali Masanja alisema, baadhi ya ndoa zimevunjia kwa kukosa uaminifu kwa sababu wanachelewa kurejea nyumbani na wanakuwa milimani kutafuta mawasiliano na kuzungumza na watoto wao waliopo mjini.

Naye Paul Mabala alisema, kunapotokea matukio mbalimbali ya kihalifu nyakati za usiku ikiwamo vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, wanashindwa kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali za mitaa na badala yake wanasubiri mpaka papambazuke na kwenda ofisini kutoa taarifa.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, akijibu malalamiko hayo alisema, katika bajeti ya mwaka huu wa fedha serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kupeleka huduma ya mawasiliano katika majimbo yasiyokuwa na mawasiliano na jimbo hilo limepewa minara saba ya mawasiliano.

Alisema, minara hiyo itajengwa katika kata saba zenye ukosefu wa huduma hiyo ambazo ni Bukomela, Bulungwa, Idahina, Nyamilangano, Ubagwe, Ulowa na Kata ya Nyankende na kwamba suala la ukosefu wa mawasiliano linakwenda kutatuliwa hivi karibuni.


Ukurasa 12

**Mdau: Katiba mpya si jambo la haraka**


Ukurasa 13

MGOMBEA RUTO AAMBIWA...
Ajiandae kuridhiana na 'swahiba'


Ukurasa 14

**MCHEZA KRIKETI IMRAN KHAN:**
**Anapotumbuliwa na Jeshi la Pakistan**


siasa

JUMATANO MEI 4, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


# CHADEMA yaombwa kujitizama tena, lakini kupunguza ukali

**Na Sabato Kasika**

SIKU chache baada ya CHADEMA kusita kutoa maoni kwenye kikao cha Kikosi Kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan cha kupokea mapendekezo katika maeneo kadhaa ikiwamo katiba, chama hicho kimeshauriwa kubadili msamamo huo mkali kwa manufaa ya Watanzania.

Katibu wa Kikosi Kazi cha Rais Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, wiki iliyopita alisema, chama hicho ni moja ya vyama vya siasa vinavyotarajiwa kutoa maoni na mapendekezo yao Mei 9, mwaka huu, lakini kilitoa msimamo unaoonyesha kutokuwa tayari.

Chama kinadai hakitakuwa tayari kushiriki katika kikao hadi kuwe na makubaliano ya wapi pa kuanzia na ajenda za mazungumzo ziwe wazi.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam, Abbas Mwalimu, anasema, kinachofanywa na CHADEMA ni siasa za kuviziana na kushauri viongozi wake kubadilisha msimamo kwa manufaa ya umma.

"Busara iwaongoze viongozi wa chama hicho kushiriki mchakato unaoendelea wa kutaka kupatikana katiba mpya, kwani kususia ni sawa na kupoteza nafasi ya kutoa maoni na maduku duku yao," anasema Mwalimu.

Siasa za kuviziana na kutafuta sababu za kukwamisha mchakato huo siyo jambo jema, badala yake wadau washirikiane ili kuhakikisha nchi inapata katiba, kwa kutoa maoni yanayohitajika, anasema Mwalimu.

"Lengo kuu la katiba ni kuleta ustawi kwa wananchi, lakini wanasiasa watazama sehemu yao yenye maslahi kwao, wanasahau kuwa inagusa ustawi wa


Mkurugenzi wa Uenezi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, akisema chama hakijaridhia kutoa maoni. **PICHA: MTANDAO**

jamii, usalama, utamaduni na pia uboreshaji wa huduma za umma. Watoe maoni badala ya kuendelea kutoa visingizio kila wakati."

Anafafanua kuwa suala la kuwapo kwa katiba linategemea utashi wa Rais na kwamba Rais Samia, ameonyesha utayari huo akiwataka wanaosusa kuacha mambo hayo.

"Nikumbushe kuwa kupata katiba kunahitajika utafiti kisayansi, ikiwamo kujifunza kwa wengine walivyofanikiwa kutengeneza katiba yao au ni wapi wamekwama ili kuwe na pa kuanzia. Yote yanahitaji ushirikiano," anasema Mwalimu.

**HAKI KIDEMOKRASIA**

Mwana harakati, mtetezi wa haki za binadamu Dk. Helen Kijo-Bisimba, anasema, hivyo ndivyo demokrasia ilivyo, kwamba msimamo wa chama hicho ni jambo la kawaida katika siasa, na kwamba la muhimu uwe na mashiko.

Anafafanua kuwa hajazizingatia sababu zinazokifanya chama hicho kutoshiriki vikao vinavyoandaliwa na kikosi kazi, bali anachojua ni kwamba, kila mmoja ana haki ya kukataa au kukubali jambo kulingana na jinsi anavyoliona.

"Sioni tatizo kama kuna sababu za msingi za viongozi wa chama hicho kukataa kushiriki vikao vya kikosi kazi kilichoundwa kutafuta katiba bali ninachukulia kama haki yao kidemokrasia," anasisitiza Dk. Kijo-Bisimba.

Anaongeza kuwa, kinachotakiwa kufanywa na wadau au Kikosi Kazi hicho ni kuchambua hoja za chama hicho ili kuona zina uzito gani, kwa maelezo kwamba viongozi wa chama hicho wanaweza kuwa na hoja za msingi.

"Kwanza tujiulize, CHADEMA wamekuwa mstari wa mbele kudai katiba mpya, wamepewa nafasi kupitia Kikosi Kazi, lakini wanakataa, kwa nini? Inawezekana wana sababu za msingi," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu huyo wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), anasema suala katiba mpya linahitaji maridhiano, na kwamba iwapo baadhi ya watu wakikataa kushiriki mchakato, huwa kuna jambo haliko sawa.

**MSIMAMO WA CHADEMA**

Baada ya kutangazwa kwa kikao hicho wiki iliyopita, Nipashe ilizungumza na Mkurugenzi wa Uenezi na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, ambaye alisema chama hakijabadili msimamo.

"Kama ambavyo Kamati Kuu iliazimia kuhusu kutoshiriki mchakato huo, hadi sasa hakuna uamuzi uliobadilika na tuna imani kuwa tutaweza kufanya mazungumzo kwanza ili tukubaliane tunaanzia wapi na ajenda za mazungumzo zitakuwa zipi.


"Tumemsikia mheshimiwa Rais alipokuwa Marekani aliweka wazi kuwa ataendeleza mazungumzo hayo, nasi tutakuwa tayari kuendelea baada ya kuweka misingi ya mazungumzo husika."

Wakati chama kikiwa na msimamo huo, taarifa ya Kikosi Kazi inaonyeha kuwa maoni na mapendekezo ya wananchi na taasisi katika maeneo hayo tisa

**INAENDELEA UK. 13**

# Mdau anena Katiba Mpya si jambo la haraka wala papara

• Unahitajika muda kuchambua, kufikia uamuzi



Baadhi ya wajumbe wa Bunge Maalumu la Katiba lililokutana karibu miaka minane iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

**Na Faustin Sungura**

SAUTI mbalimbali zinaibuka kuzungumzia Tanzania kuwa na katiba mpya kumekuwa na maoni ya wadau wengi kuhitaji katiba mpya sasa au kuboresha iliyoko, lakini wapo wanaotaka kuiacha iliyoko iendelee kutumika.

Licha ya kwamba wapo wengine wanaitaka katiba mpya cha kushangaza wanairejea rasimu iliyoandaliwa na Tume ya Jaji Warioba kwa maelezo kuwa ni ili mchakato wake uendelezwe na kukamilika na kuipatia nchi andiko jipya. Itakumbukwa kuwa wakati wa mchakato wa kuandaa rasimu hiyo, kulijitokeza makundi mawili ya waliokuwa wanataka ipitishwe na wengine wakiipinga kuwa imehujumiwa na wingi wa waliokuwa wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba lililokutana 2014.

Wakati ule wa Bunge Maalum la Katiba, ilishuhudiwa baadhi ya wajumbe waliotoka vyama vya NCCR-MAGEUZI, CHADEMA, CUF na NLD chini ya mwavuli wa UKAWA - Umoja wa Katiba ya Wananchi wakisusia bunge hilo na kutoka nje ya vikao.

Wakati huo wajumbe waliotokana na vyama vya CCM, TADEA, AAFP, NRA, CCK na wawakilishi wa taasisi za kijamii wakiendelea na vikao hata kuipitisha rasimu iliyopo ya katiba pendekezwa kwa hatua zingine.

> Jambo jingine ni kuunda tume ya kukusanya maoni ya wananchi, kuyachambua, kuyachuja na kuandaa chapisho pengine kazi hiyo inaweza kuchukua kati ya miaka miwili mpaka mitatu.

Sasa ni takribani miaka nane tangu Bunge Maalum la Katiba liifanye kazi yake, vyama vya NCCR-MAGEUZI, CHADEMA, CUF na baadhi ya taasisi na asasi za kijamii, wanaongoza kijiti cha kutaka katiba mpya ipatikane kabla au mwaka mmoja baada ya 2025.

Kazi ya kusoma, kufikiri, kuchambua na kuandika ni ngumu ni kazi inayohitaji muda, utulivu na uvumilivu. Nimepitia kazi ngumu ya Tume ya Warioba, kuanzia rasimu ya kwanza hadi katiba inayopendekezwa; wamefanya jukumu gumu, nzuri na ninawapongeza.

Hata hivyo, rasimu yao mbali na kuwa na mambo mazuri, inayo mapungufu ambayo kwa mtazamo wangu nilidhani yanahitaji mjadala mkubwa. Mathalani, rasimu inapendekeza kuwapo na uwakilishi wa 50/50 kwa wanaume na wanawake kwenye nafasi za uongozi.

Si vibaya kujiuliza, ni kwa nini iwe kwenye uongozi pekee? Lakini inapendekeza kuwapo kwa Mahakama ya Juu (Suprime Court) ni kwa nini? Siyo kufanya mchujo kwa Majaji na Mahakimu ili kujua ubora wa utendaji kazi wao kabla ya kuwaongezea mzigo mzito walipa kodi kwa kuanzisha mahakama nyingine?

Kwa kuwa muda mrefu umepita bila rasimu ya katiba kupitishwa, ni matarajio yangu kuwa jamii ya Watanzania itakuwa imejifunza au kuona uhitaji wa baadhi ya mambo mengine ya kuzingatiwa katika katiba ijayo.

Moja ya mambo ya kujadili ni tukio la iwapo nchi itampoteza rais aliyeko madarakani. Ni eneo la kujadili kuhusu je, taifa liendelee na utaratibu uliopo wa Makamu wa Rais kuirithi nafasi hiyo? Watanzania wanaweza kulichambua jambo hilo kwa kurejea mazingira waliyo nayo. Je, iwapo Rais na Makamu wake watapoteza maisha inakuwaje? Katiba izungumze pia.

Suala la katiba mpya limekuwa gumzo hata kwa awamu ya sita na mwaka jana Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa msimamo wake kwamba, suala la katiba mpya mpya litaanza kufanyiwa kazi baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Walio na haraka ya katiba wanahoji ni kwa nini taifa liendelee kusubiri? Wasio na haraka nayo wamesema hewala. Kutokana na uzoefu wangu kwenye siasa na mazingira ya nchi hii na watu wake ninaungana na wale wasio na haraka ya kuwa na katiba mpya.

Kwa mtazamo kwamba inaonekana kuwa mchakato wa kuipata au marekebisho ya katiba ya sasa, unatakiwa kuanzwa upya. Ikimaanisha kwamba inayoitwa Katiba ya Warioba na timu yake haitakuwa na nafasi wala huenda haitalifaa tena taifa kwa sababu, hapakuwa na maandalizi mujarabu na ya kikamilifu kwa wananchi kutoa maoni yao.

Kwa mtazamo huo mchakato wa kupata au katiba mpya au kufanya marekebisho ya katiba ya sasa, unatakiwa kuchukua si chini ya miaka minne hata nane.

Wengi wanaweza kukubaliana nami kuwa mchakato wa kupata katiba unatakiwa kuendana na kuchapisha nakala nyingi za katiba ya sasa na kuzisambaza kwa wananchi kwa gharama ndogo pengine ya Shilingi 500 hadi 700 ili waisome na kazi hii inaweza kutuchukua miaka kadhaa.

Eneo jingine ni kuwapa wananchi muda wa kutosha wa kusoma katiba ya sasa, ili waweze kubaini mazuri, mabaya, udhaifu, upungufu na viraka vilivyo katika katiba hiyo pengine kazi hiyo ikichukua miaka mitatu hadi minne.

Jambo jingine ni kuunda tume ya kukusanya maoni ya wananchi, kuyachambua, kuyachuja na kuandaa chapisho pengine kazi hiyo inaweza kuchukua kati ya miaka miwili mpaka mitatu.

Aidha, wananchi wanahitaji pia kuhakiki maoni yao chini ya jopo la wataalamu wa fani mbalimbali miaka miwili hadi mitatu inaweza kutumika kufanikisha lengo hilo.

Huenda jamii itakubaliana nami kwamba, katiba mpya au marekebisho ya katiba ya sasa inaweza kuwa yenye manufaa kwa wananchi, kama raia wanaotoa maoni juu ya katiba, wamewahi kuiona na kuisoma iliyopo, kwa wao kuiona na kuisoma ni kupata nafasi chanya kwa watu wanaokusanya maoni yao, kujua wamekutana na watu wa aina gani.

Aidha, tume ya maoni itafahamu ni wangapi wanajua kusoma na kuandika na wangapi hawajui kusoma au kuandika, itafahamu idadi ya waliowahi kuiona na kuisoma katiba iliyopo; wangapi hawajawahi kuiona na wala hawaifahamu.

Halikadhalika wangapi wameisoma katiba iliyopo; wangapi wanataka au hawataki katiba mpya kwa sababu zipi au wamesikia chama chao kinataka au hakitaki katiba mpya.

Ni imani yangu kuwa serikali inatakiwa, kabla ya kuteua tume ya maoni, itawaandaa wananchi wake kwa kuhakikisha hicho wanachokitolea maoni wanakijua kwa ukamilifu na siyo vinginevyo ili mchakato wa katiba mpya ueleweke, ukubalike na ufahamike na ushirikishe Watanzania wengi .

***Maoni: 0769-66 82 84 au faustinsungura8@gmail.com***

MGOMBEA RUTO AAMBIWA...

# Ajiandae kuridhiana na 'swahiba' wake Raila baada uchaguzi mkuu

• Angalizo kutoka Katibu Mkuu Wizara Ulinzi

**Na MWandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ulinzi ya Kenya, Eugene Wamalwa, amemwambia Naibu Rais wa Kenya William Ruto, ajiandae kwa maridhiano na mgombea urais Raila Odinga, kazi atakayoifanya baada ya uchaguzi mkuu wa Agosti mwaka huu kumalizika.

Raila anagombea urais kupitia Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya, wakati Ruto anagombea kupitia United Democratic Party Alliance (UDA) licha ya kwanza aliingia ikulu kupitia Muungano wa Jubilee.

Anatoa ujumbe huo Jumapili katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Kizito lililoko Magemo katika wadi ya Ndivisi, kwenye Jimbo la Webuye Mashariki, wakati wa harambee ya kuchangia fedha kwa ajili ya kanisa hilo, Wamalwa alimwambia Dk. Ruto kuwa maandishi yako ukutani kwamba Raila Odinga atakuwa Rais wa tano wa Kenya.

Eugene Wamalwa ambaye ni mdogo wa aliyekuwa Makamu wa Rais wa Kenya wakati wa awamu ya Mwai Kibaki, marehemu Michael Kijana Wamalwa, amemwambia Ruto achunge mwenendo wake kwani ana uhakika 'Odinga anakuwa Rais wa Tano wa Kenya' na hilo halina ubishi.

Aidha, Eugene Wamalwa akiwa pamoja na Naibu Mwenyekiti wa Muungano wa Jubilee, David Murathe, alimkosoa Dk. Ruto Jumamosi, wakati wa mazishi ya marehemu Rais Mwai Kibaki huko Othaya, Kaunti ya Nyeri, kuwa haungi mkono siasa za upatanishi na kupeana mikono ya maridhiano.

Anasema Odinga muda wote wa maisha yake ya kisiasa ameweka kando dhamira na nia yake ya mambo binafsi kwa kuyaweka mbele maslahi ya Kenya hata pale alipoporwa ushindi wake alikaa kimya na kumtaka Dk. Ruto, kufuata nyayo zake.

"Nilivurugwa na kukerekwa nilipoona Ruto anakataa hata kusalimiana na viongozi wenzake wakati wa mazishi ya Kibaki tena mbele ya bosi wake Rais Uhuru Kenyatta. Hiyo ni dharau, wakati Wakenya wengi wanafahamu kwamba maridhiano siku za nyuma ndiyo silaha iliyoleta amani hapa nchini," anasema.

Kama njia ya kumuenzi marehemu Rais Mwai Kibaki, Ruto endapo atashindwa na Odinga katika uchaguzi mkuu ujao, ambao sina shaka ataanguka akubali kushindwa na amfikie Odinga ili ampe mkono wa maridhiano na kukumbatiana, ili kuendeleza amani na mshikamano wa nchi yetu," anasema Wamalwa.



Eugene Wamalwa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi, alipomwambia Ruto 'maandishi yako ukutani Raila ndiye Rais wa Kenya ajaye'. **PICHA: DAILY NATION**

Wamalwa anakumbusha kuwa muafaka wa 2007 kati ya Mwai Kibaki na Raila Odinga uliIeta utulivu baada ya uchaguzi mkuu uliovurugwa.

"Watu wengi walipoteza maisha, mali za mamilioni ziliharibiwa huku biashara zikishuka. Kenya ilikuwa ikikaribia kuporomoka kabla ya wawili hao kupeana mkono wa mardhiano ili kunusuru nchi," anakumbusha, akitetea mapatano kati ya viongozi hao wawili wa kisiasa.

Katibu Mkuu wa Waziri wa Ulinzi anasema hali kama hiyo ilishuhudiwa 2018 wakati Rais Uhuru Kenyatta na Odinga walipopeana mkono wa maridhiano na kutuliza nchi, tena baada ya uchaguzi uliovurugwa na kukumbwa na malalamiko mengi.

"Natoa wito kwa wagombea hawa wawili wa urais kwamba yeyote atakayeshindwa ajiandae kufanya kazi na mwenzake katika mazingira ya kukubaliana na kuwa na maridhiano kwa kupeana mkono," anasema Wamalwa.

Wamalwa anakumbusha kuwa alifanya kazi na Rais Mwai Kibaki na kumkumbuka kama rais aliyesaidia nchi kupata katiba mpya.

"Kibaki na Raila walifanya kazi pamoja kuleta katiba mpya iliyoshuhudia Wakenya milioni saba wakipiga kura ya ndiyo, huku watu milioni tatu wakiongozwa na Dk. Ruto wakipiga kura ya hapana na hiyo ina maana ni Raila pekee anayeweza kulinda mabadiliko na kuwapa wananchi madaraka kwenye serikali za mitaa yaliyoletwa na katiba mpya," anasema.

> Murathe anamuonya Ruto kuwa kwa sababu ya kutomheshimu Rais Kenyatta, hatakuwa Rais wa taifa hilo.

Wakati huo huo, Murathe amesema ni zama za mtu ambaye si Mkikuyu na asiye Mkalenjin kuongoza nchi.

Aidha anasema mara kadhaa Rais Kenyatta, alimtaka Dk. Ruto kujiuzulu iwapo haridhishwi na serikali yake.

"Uhuru alituambia sisi tulio katika Muungano wa Jubilee kwamba Ruto anastahili kujiuzulu na tunaweza kuwa na Eugene Wamalwa hapa awe Naibu Rais kwa sababu ya ujuzi mkubwa na sifa za uongozi alizo nazo," anasema Murathe.

"Tunashangaa kwa nini Ruto anaendelea kupata marupurupu yote ya serikali kama kiongozi, ilhali anaendelea anamtusi Rais Kenyatta bila aibu. Tuliona Jaramogi Odinga akijiuzulu kama makamu wa rais, akisema angeweza kuhalalisha mshahara wake wakati hawezi kufanya kazi na Baba wa Taifa wa Kenya, Rais Mzee Jomo Kenyatta.

Murathe anamuonya Ruto kuwa kwa sababu ya kutomheshimu Rais Kenyatta, hatakuwa Rais wa taifa hilo.

"Hivi karibuni tutaanza kuzunguka nchi hii na Uhuru, tukiwaambia wapigakura kile kilicholeta mpasuko kati ya viongozi hao wawili," anasema.

Anaongeza: "Sote tulimsikia Rais Uhuru akisema ni wakati wa jamii nyingine kutawala na kuongoza nchi hii badala ya Wakikuyu na Wakalenjin, na wakati huu sisi Wakikuyu tutampigia kura Odinga kama anavyosema Rais," anaeleza.

Akihitimisha, Katibu Mkuu huyo aliwataka wapigakura Magharibi mwa Kenya kukumbatia amani kabla ya uchaguzi wa Agosti mwaka huu.

"Mulembe ni amani ... na tunataka kuwahimiza viongozi wetu kuepuka siasa za kurudi nyuma na za chuki zinazoweza kusambaratisha nchi," anaonya, akiwataka viongozi wa kidini kuliombea taifa na Dk. Ruto kuwa na moyo wa kuomba radhi ili akubali kushindwa na kupeana mkono na Odinga iwapo atashindwa kwenye uchaguzi mkuu."

Aidha, Murathe anaitaka timu ya Azimio kushirikiana na kukubaliana kusimamisha mgombea mmoja katika maeneo ambayo wana zaidi ya mmoja ili kuepuka kuangushwa na wagombea wengine.

***Mtandao***

## CHADEMA yaombwa kujitizama tena, lakini kupunguza ukali

**INATOKA UK. 11**

yatapokewa jijini Dar es Salaam kuanzia kesho hadi Mei 13, mwaka huu.

Ratiba hiyo pia inaonyesha kuwa kesho watakaoanza kutoa maoni na mapendekezo ni CCM), ACT-Wazalendo na kufuatiwa na Chama cha Union for Multiparty Democracy (UMD).

Mei 6 itakuwa siku ya CUF, NCCR-Mageuzi kutoa maoni yao na siku itakayofuata (Mei 7) ni Jumuiya ya Wahindu Tanzania na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT).

Mei 9 itakuwa nafasi kwa CHADEMA, ADC, Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) huku kesho yake vikifuatia vyama vya United Peoples Democratic Party (UPDP), African Democratic Alliance Party (ADA-TADEA) na Alliance for African Farmers Party (AAFP) na vingine vyote.

Masuala yanayojadiliwa na Kikosi Kazi ni pamoja na katiba mpya, mengine yanayotolewa maoni na mapendekezo ni mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya vyama vya siasa, uchaguzi na elimu ya uraia.

Mengine ni mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na umoja wa kitaifa na ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa na demokrasia ya vyama vya siasa.

Rushwa, maadili katika siasa na uchaguzi, ruzuku ya serikali kwa vyama vya siasa na uhusiano wa siasa na mawasiliano kwa umma pia yanatakiwa kutolewa maoni na wadau hao.

JUKWAA LA UONGOZI

MWANA KRIKETI IMRAN KHAN:

# Waziri Mkuu aliyetumbuliwa na Jeshi Pakistan, alipobuni mapya

• Alipania kuanzisha urafiki na Russia, China akakwama

**Na Ani Jozeni**

MCHEZAJI wa zamani wa kriketi wa timu ya Pakistan, Imran Khan (69) ametimuliwa kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo kazi aliyoifanya kuanzia Agosti 2018 hadi Aprili mwaka huu.

Anaondolewa kwenye madaraka baada ya bunge kuona kuwa hatoshi kwenye jukumu hilo, harakati za kumwondoa zikichochewa na jeshi.

Mwanamichezo huyo, hata leo anaendelea kuilaumu Marekani eti imechochea kumng'oa, licha ya Khan kujaribu kulizuia bunge kupiga kura ya kutokuwa na imani naye.

Khan analivunja bunge ili kufanya uchaguzi mkuu wa haraka, lakini Mahakama Kuu ya Pakistan ikazuia hatua hiyo na kulirudisha bunge kazini, likamwondoa madarakani na sasa Waziri Mkuu mpaya ni Shahbaz Sharif.

Sharif ni wa mrengo wa kihafidhina na mwanafamilia ya watawala kutoka kwa ukoo wa Nawaz Sharif.

Kaka yake Shahbaz maarufu , Nawaz Sharif aliondolewa madarakani kwa tuhuma za rushwa, kama ilivyotokea kwa mpinzani wake Asif Ali Zardari wa familia ya Zulfikar Ali Bhutto, aliyeuawa na jeshi la Pakistan, na binti yake Benazir Butto akawa Waziri Mkuu mara mbili kwa vipindi vifupi, lakini naye akauawa akiwa kwenye mkutano wa hadhara wa kampeni Desemba 2007.

Jambo la kushangaza kuhusu kampeni ya Imran Khan tangu sakata la kupigiwa kura ya kutokuwa na imani naye ni kukataa kulaumu kundi lolote nchini Pakistan au kukiri masuala yaliyokuwa yanalalamikiwa kama kuongezeka kwa bei za vitu (thamani ya rupia ilikuwa imepungua kwa asilimia 30.5 ukilinganisha na dola ya Marekani.

Aidha, kulikuwa na ongezeko la bei lililofikia asilimia 17, wakati hapa Tanzania unakadiriwa kuwa asilimia 4.7 na sababu ikiwa mikwano ya corona, mivutano ya China na Marekani, halafu sasa bei za mafuta kupaa kutokana na vita ya Ukraine na Urusi.

Licha ya Waziri Mkuu huyo kupambana na rushwa, ugumu wa maisha miongoni mwa wananchi ukamwondoa madarakani.

Kiongozi huyo kuilaumu Marekani ni kielelezo kuwa Marekani ina ushawishi mkubwa siyo katika jamii ya Pakistan ila kwa baadhi ya taasisi muhimu za nchi hiyo.

Mchambuzi mmoja akielezea hali hiyo katika majadiliano ya DW, anasema Marekani imeendelea kuungwa mkono na jeshi kutokana na kutoridhishwa na silaha au vifaa vya kijeshi alivyonunuliwa kutoka China ambavyo jeshi lake linasema ni vya viwango hafifu na likataka nyenzo za Marekani zinunuliwe.



Imran Khan katika zama zake kwenye uwanja wa kriketi. Picha chini; akiwa kwenye nyendo zake za kisiasa kwa nafasi ya Waziri Mkuu wa Pakistan. **PICHA: MTANDAO**

> Ni pale Asif Ali Zardari akielemewa na tuhuma za rushwa lakini akakosekana mwanafamilia maarufu kutoka kwenye ukoo wake kuchukua nafasi yake.



Halafu inaelekea yako 'madili' katika jeshi ambayo Imran Khan alitaka kuyazuia, akateua mkuu wa kitengo cha usalama jeshini (ISI) akipuuza ushauri wa mkuu wa majeshi wa kutaka nani ateuliwe. Ndiyo bunge likaja juu, kwa hitaji la kura ya kukosa imani kwake.

Jeshi ndilo linalosimamia kuondolewa Waziri Mkuu mwanaharakati, kama ilivyo kawaida. Hapakuwa na jipya kuwa jeshi halimtaki Khan, aliyefungamana na China na Russia kuhusu masuala muhimu ya kimataifa, likiwamo la Ukraine, kulazimisha silaha za China, huku bei ya mafuta, bidhaa muhimu zikipanda, na matajiri wanaikimbia Pakistan kutokana na sarafu kushuka thamani.

Ila kimsingi kuna tatizo la jumla la siasa nchini Pakistan kama ilivyo nchi nyingine za Asia Magharibi na Kusini, kuwa mifumo ya jamii ni ya kiukoo na kimadhehebu (kila ukoo una dhehebu au mwelekeo fulani wa kidini ambako wote wa jamii hiyo wanakuwa watiifu kwake).

Jeshi la Pakistan linawakilisha familia na mifumo ya kiuchumi na kiutawala inayoshikilia hatima za wabunge wengi, hivyo ilipofikia mahali hawataki Imran Khan aendelee kuongoza, hata wale wa chama chake hawakuwa na uwezo wa kuendelea na utii wao kwake, kama ilivyokuwa kwa Nawaz Sharif mwaka 2018, ila gurudumu la kujirudia bado linaendelea. Badala ya Nawaz kurudi madarakani licha ya tuhuma za rushwa, anaingia mwanafamilia mwingine.

Labda hicho ni kielelezo cha kuwepo aina kadhaa za demokrasia, ile ya mtu binafsi kumpigia kura anayemtaka, na demokrasia ya ukoo kama inavyoendeshwa katika nchi za Asia Magharibi na Kusini.

Ndiyo hapo zinazaliwa familia za utawala kama za kina Bhutto au kina Nehru nchini India ambao sasa hivi hawako madarakani. Lakini wana nguvu kwani Rahul Gandhi, mjukuu wa Waziri Mkuu Indira Gandhi aliyeongoza baada ya baba yake Jawaharlal Nehru, aliyeleta uhuru India, leo ndiye kiongozi wa upinzani.

Mfumo huo wa kifamilia hutokea viongozi wapya, kama mhafidhina Narendra Modi nchini India kwa sasa, au Imran Khan aliyejumuisha harakati za dini kuchanganya na zile za mabadiliko kijamii.

Ni pale Asif Ali Zardari akielemewa na tuhuma za rushwa lakini akakosekana mwanafamilia maarufu kutoka kwenye ukoo wake kuchukua nafasi yake.

Kinachoonekana kwa wachambuzi wa habari ni kukwama kwa Imran Khan aliyekuwa akitegemea nguvu ya umma dhidi ya jeshi, akiweka matumaini makubwa katika madaraka yake kikatiba kufanya uteuzi anavyotaka. Alitazamia kuwa wananchi wa Pakistan wataelewa anachokifanya hasa katika kupambana na rushwa, asigundue kuwa watu wanachokitaka ni maisha bora, bei rahisi za vitu, na siyo kampeni dhidi ya rushwa wala chochote kingine.

Isitoshe aliweka mkazo katika siasa za kuichukia Marekani, kupinga uingiliaji wake katika nchi kadhaa ambazo wanaziunga mkono kiitikadi. Kama Libya akipinga marekani ilivyomwondoa Muamar Gadaff

Na bado Khan ni miongoni mwa wanaokerwa na kile alichofanyiwa Saddam Hussein, licha ya kuwa kulikuwa na madai mengi ya kukomsoa kama kuwakata wapinzani wake masikio hospitalini, na raia wake wa kaskazini (Wakurdi) na kusini (Washia) walikuwa wanalindwa na vikosi vya Marekani na Uingereza walioweka 'no fly zone' (zuio la kutumia anga kwa ndege za kijeshi) ili raia hao wasiteswe.

Yote hayo hayakukubalika kwa wanaharakati na Imarn Khan alifanya kila juhudi kuwaridhisha.





# Taasisi zinazokiuka eGA kuchukuliwa hatua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (eGA), imetakiwa kuzichukulia hatua stahiki taasisi zote za umma zinazokiuka matakwa ya Sheria ya Serikali Mtandao namba 10 ya mwaka 2019.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alitoa agizo hilo juzi jijini hapo alipokuwa akifunga kikao kazi cha Wakuu wa Idara na Vitengo vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) serikalini kilichohusu mafunzo ya uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Serikali Mtandao (eGA).

Alisema eGA ni mamlaka kamili hivyo, inapaswa kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria pale inapoona taasisi za umma zinajenga mifumo ya TEHAMA bila kibali cha mamlaka hiyo au zinapokiuka sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya serikali mtandao.

"eGA mna meno kisheria hivyo anzeni kuitekeleza Sheria ya Serikali Mtandao kwa vitendo kwa kuzichukulia hatua mara moja taasisi zote zinazokwenda kinyume na sheria hiyo," alisema.

Kuhusu malalamiko ya upatikanaji wa mtandao kwenye baadhi ya maeneo, Ndejembi aliwataka wakuu hao kutafuta suluhisho la tatizo hilo ambalo wananchi wamekuwa wakilalamikia wanapohitaji huduma zinazotolewa na Taasisi za Umma kupitia mifumo ya TEHAMA.

"Unakuta mwananchi anatembea umbali mrefu kufuata huduma ya kulipa kodi kwa manufaa ya taifa, halafu anaambiwa mtandao hakuna kwani mfumo haufanyi kazi, na wakati mwingine kwenye halmashauri zetu kutengeneza namba ya malipo mwananchi anaambiwa mtandao uko chini jambo ambalo linakwamisha utoaji wa huduma," alisema.

Alisema kipaumbele kikubwa cha serikali ni kuwa na Serikali ya Kidijitali itakayoondoa matatizo ya wananchi kutopata huduma bora na kwa wakati hivyo na kuwaasa wataalamu wa TEHAMA kutumia ujuzi wao kujenga mifumo imara itakayoboresha utoaji wa huduma.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Mhandisi Benedict Ndomba, alimhakikishia Ndejembi kuwa, eGA itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za serikali mtandao kwa taasisi za umma na kuhimiza uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo ya serikali mtandao.

Kikao kazi hicho cha siku mbili kimehudhuriwa na Wakurugenzi wa TEHAMA wa wizara, Wakuu wa TEHAMA wa idara zinazojitegemea, Mamlaka na Wakala za Serikali, Wakuu wa vitengo vya TEHAMA wa Mikoa, Majiji na Manispaa, Wakuu wa vitengo vya TEHAMA wa halmashauri za wilaya na wakuu wa TEHAMA wa Taasisi za Umma.



Waumini wa dini ya kiislamu wakishiriki swala ya Eid El Fitr katika msikiti wa Gadafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wakazi wakumbushwa kuikijanisha Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI wa jijini Dodoma, wametakiwa kuendelea kutunza na kupanda miti kwa wingi ili kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuikijanisha Dodoma.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Mkoa wa Dodoma, Ahidi Sinene, alitoa kauli hiyo jana kwenye upandaji miti 2,000 katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, jijini humo.

Sinene alisema kila mwananchi anapaswa kutambua jitihada zinazofanywa na serikali za kuboresha mazingira nchini, hivyo ni vyema kila mmoja kuwajibika kupanda miti ya kutosha kwenye mazingira anayoishi ili kustawisha maeneo hayo.

"Nasisitiza wana-Dodoma tujikite katika suala la kupanda miti kwa sababu inasaidia kuondoa ukame, ikiwamo kuleta kivuli hususani msimu wa kiangazi," alisema Sinene.

Alitaka hospitali hiyo kuitunza miti hiyo ili kusaidia kutimiza kampeni ya Rais Samia ya kuikijanisha Dodoma.

"Tunapopanda miti kutimiza ndoto ya kuikijanisha Dodoma na mikoa mingine, lakini tuna support (tunaunga) jitihada za Rais Samia za kusisitiza suala la uboreshwaji wa mazingira," alisema Sinene.

Naye Katibu wa Taasisi ya Habari Development Association inayojishughulisha na upandaji miti ambao ndio waandaaji wa zoezi hilo, Bernard James, alisema hivi sasa wamejikita kuikijanisha Dodoma kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira uliofanywa.

Alisema, wameitikia maagizo ya Rais Samia ya kutunza mazingira huku akiitaka hospitali hiyo kutunza miti 2,000 iliopandwa eneo hilo ikiwamo ya matunda kwa udhamini wa Bakhresa Group. Alisema wanaamini miti hiyo itatunzwa kwa kumwagiliwa vizuri ili kutimiza lengo lililokusudiwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Sheria na Utawala kutoka Bakhresa Group, Shani Mligo, alisema harakati hizo za upandaji miti zinapaswa kuwa endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

"Tunaomba taasisi nyingine ziige mfano wa Habari Development Association, tunahitaji kuona Tanzania inazidi kuwa ya kijani," alisema Mligo.

# Mtaka ataka uadilifu utunzaji kumbukumbu nyaraka za serikali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka watunza kumbukumbu na nyaraka za serikali kuzingatia uadilifu, kanuni, taratibu na miongozo inayotolewa na serikali ili kurahisisha utendaji kazi wao.

Mtaka aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo kwenye kikao kazi cha watunza kumbukumbu hao kilicholenga kujadili masuala ya utunzaji wa kumbukumbu katika utumishi wa umma.

"Uadilifu katika kutekeleza majukumu yetu ni jambo la msingi sana hivyo kwa wale ambao si waadilifu wabadilike ili tuweze kuwa na mchango katika kujenga utumishi wa umma ulitukuka," alisema.

"Najua kuna changamoto nyingi mnakutana nazo maofisini kwenu na nyingine mmezitaja hapa, hivyo basi msiache kuwa waadilifu hata kama viongozi wenu watakuwa hawawathamini."

Mtaka alikemea tabia ya baadhi ya viongozi kufanya masjala ni kama sehemu ya kuwaweka watu kutumikia adhabu wanazopewa endapo wakifanya makosa.

"Masjala sio sehemu ya mtu kutumikia adhabu kwa mtumishi wa juu aliyefanya kosa, haiwezekani kumpeleka mtu ambaye hana taaluma ya utunzaji kumbukumbu akafanye kazi ya kutunza kumbukumbu," alisema Mtaka.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Taaluma ya Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania (TRAMPA), Francis Mathias, aliahidi kufanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na mkuu huyo wa utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika taasisi za umma uwe na manufaa katika utendaji kazi wa taasisi na kwa maendeleo ya taifa.



# Watumiaji bidhaa za tumbaku wahadharishwa

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imewatahadharisha wananchi wanaotumia bidhaa mbalimbali za tumbaku kupunguza matumizi kwa kuwa zina madhara kiafya.

Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti wa Dawa wa TMDA, Dk. Yonah Mwalwisi, alitoa tahadhari hiyo hivi karibuni wakati wa mafunzo maalumu kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Mbeya, Njombe, Songwe na Rukwa yaliyofanyika jijini hapo.

Alisema bidhaa za tumbaku zina madhara mbalimbali ya kiafya kwa binadamu ndiyo maana serikali kupitia TMDA kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa likiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO), inadhibiti matumizi ya bidhaa hizo.

Kwa mujibu wa Dk. Mwalwisi, kwa wanawake, bidhaa za tumbaku husababisha saratani ya mfuko wa uzazi, mwanamke kushindwa kushika mimba, kuzaa mtoto aliyekufa, mimba kutoka na baadhi huwasababishia utasa kabisa na hivyo kutokuwa na uwezekano wa kuzaa kabisa.

Dk. Mwalwisi alisema kwa wanaume, bidhaa hizo husababisha upungufu wa nguvu za kiume kutokana na kuharibu mzunguko wa damu.

"Mbegu za kiume zikiharibika huwa kunakuwa na uwezekano wa mtoto atakayezaliwa na mwanamume huyo kuwa na uwezekano wa kupata magonjwa ya saratani," alisema Dk. Mwalwisi.

Kuhusu watoto, alisema matumizi ya bidhaa za tumbaku husababisha zaidi ya nusu ya vifo vya watoto wachanga na kusababisha baadhi ya viungo vya watoto kuharibika kabisa, hivyo kuwa miongoni mwa vyanzo vya ulemavu.

Alisema moshi wa tumbaku husababisha huathiri mfumo wa upumuaji kwa watoto pamoja na kuharibu mfumo wa hewa unaosababisha miili yao kudhoofu.

Kwa sasa, alisema matumizi ya bidhaa za tumbaku yamekuwa yakiongezeka kwenye mataifa yanayoendelea huku yakipungua kwa mataifa yanayoendelea yakiwamo ya Bara la Afrika hali ambayo alisema inasababisha ongezeko la madhara.

"Magonjwa yatokanayo na bidhaa za tumbaku yanaigharimu WHO Dola za Kimarekani Trilioni 1.4, lakini ni asilimia 20 pekee ya nchi duniani ambayo yamefanikiwa kupunguza matumizi ya bidhaa za tumbaku," alisema Dk. Mwalwisi.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema matumizi ya tumbaku yamekuwa na madhara makubwa kwa jamii, hivyo akawaomba TMDA kuendelea kuhamasisha matumizi hayo kupungua.

Homera alisema Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo imekuwa ikifaidika na kilimo cha tumbaku lakini kuna kila haja ya kuanza kuwahamasisha wakulima kuanza kuzalisha mazao mbadala ili waachane na kilimo hicho.

Alisema elimu inatakiwa iendelee kutolewa kwa wananchi ili waache kutumia bidhaa hizo na kuepuka madhara ya matumizi ya bidhaa hizo hasa uvutaji wa sigara na shisha.

Bidhaa za tumbaku ambazo zimekuwa zikitumika zaidi nchini ni sigara, shisha, ugoro, siga na tumbaku iliyowekwa kwenye bomba maarufu kwa jina la kiko.



Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Ushirika wa Mbalizi katika Dayosisi ya Konde, Mchungaji Usweghe Mwamasinga, akisoma tamko la wachungaji wa kanisa hilo, la kuendelea kumtambua aliyekuwa Askofu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali, 'aliyeng'olewa'. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Walimu waliokaa muda mrefu wahamishwa

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

HALMASHAURI ya Busokelo, Rungwe mkoani Mbeya, imeanza kuwaondoa baadhi ya walimu waliokaa kwa muda mrefu kwenye baadhi ya shule baada ya kubaini kuwa wamekuwa chanzo cha kushuka kwa taaluma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Loema Peter, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo. Alisema kwa kuanzia wameanza na Shule ya Sekondari Lwangwa.

Alisema miaka ya nyuma shule hiyo ilikuwa inafanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa lakini kwa miaka ya karibuni imeporomoka kupita kiasi hali iliyoilazimu halmashauri kuanza kuchunguza chanzo cha kushuka huko kitaaluma.

Mkurugenzi huyo alisema walibaini kuwa baadhi ya walimu wa shule hiyo pamoja na zingine zilizoshuka kitaaluma, wamekaa muda mrefu hali inayowafanya wawe wanafanya kazi kwa mazoea.

"Baadhi ya walimu hao tumewapeleka kwenye shule zingine na wale ambao walikuwa bado ni wageni tumewaacha waendelee kufundisha. Lakini tumetoa tahadhari kwao na tutaendelea kufuatilia na shule zingine," alisema Loema.

Alisema mbali na walimu kukaa muda mrefu pia wamebaini kuwa baadhi ya shule zimeshuka kitaaluma kutokana na wanafunzi kutopata chakula cha mchana shuleni.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Anyosisye Njobelo, aliwataka madiwani wa kutembelea shule zilizoko kwenye kata zao mara kwa mara ili kujua matatizo yanayozikabili na kushiriki kutatua matatizo hayo.

Aliwataka madiwani hao kuwa mstari wa mbele kuchangia chakula kwa ajili ya wanafunzi ili kuwahamasisha na wananchi wengine kuchangia ili wanafunzi wawe wanakula chakula cha mchana.

"Tusiwe tunawalaumu walimu pekee lakini na sisi madiwani tunatakiwa tushiriki kutatua matatizo ya shule zetu, tuwe tunazitembelea na kuangalia matatizo yanayozikabili," alisema Njobelo.

Busokelo ni moja ya halmashauri za mkoa wa Mbeya ambazo katika miaka ya karibuni zimeshuka kitaaluma na kusababisha serikali kuanza kuchukua hatua.

# RC awaombea misaada waathirika mafuriko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema mafuriko yaliyotokea wilayani Kyela kuanzia Aprili 27 mpaka 29, mwaka huu, yameathiri zaidi ya wananchi 1,500 ambao baadhi nyumba zao zimebomoka na wengine wamepoteza mazao na mifugo kwa kusombwa na maji.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo jana jijini Mbeya alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu tathmini ya maafa yaliyosababishwa na mafuriko hayo.

Alisema katika tathmini waliyoifanya wamebaini zaidi ya nyumba 300 zimebomoka kabisa na mali zilizokuwamo zimeharibika au kusombwa na mafuriko hayo na kwamba mpaka sasa vifo bado ni vitatu vilivyoripotiwa tangu wiki iliyopita.

Homera alisema mafuriko hayo yameathiri vijiji 41 vya wilaya hiyo na kwamba yalisababishwa na kufurika kwa mito ya Songwe, Kiwira na Mbaka.

Alisema baada ya kumaliza kufanya tathmini hiyo, waliandika barua na kuituma Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa kuomba msaada kwa ajili ya waathirika.

"Katika ofisi yetu ya maafa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo makao makuu yake yako hapa Mbeya, kuna magodoro, mablanketi, mashuka na mikeka. Tunaangalia namna ya kuyachukua na kwenda kuwasaidia wananchi hawa baada ya kupata kibali kutoka katika Ofisi ya Waziri Mkuu," alisema Homera.

Alisema mbali na vifaa hivyo vya kulalia pia wanahitaji msaada wa zaidi ya tani tano za chakula, mahema 41 kwa ajili ya wananchi waliohifadhiwa kwenye kambi zilizotengwa na vitu vingine vidogo vidogo.

Homera aliwaomba Watanzania wenye uwezo kutshirikiana na serikali kuwafariji wananchi hao kwa kutoa misaada mbalimbali hasa chakula na vifaa vya kulalia akisisitiza kuwa hali bado ni tete kwa wananchi hao.

Wilaya ya Kyela imekuwa ikikumbwa na mafuriko ya mara kwa mara na mara nyingi yanatokana na mvua inayokuwa ikinyesha katika wilaya za Rungwe na Ileje mkoani Songwe na kwa mwaka huu, yameua watu watatu na kuwaacha zaidi ya 1,500 bila makazi.





# Waziri aelezea manufaa mtandao 'Sema na Rais'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, amesema kitendo cha Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kufanya mazungumzo na vyombo vya habari kila mwezi pamoja na kuzindua mtandao wa kufanya mawasiliano na Rais 'Sema na Rais Mwinyi' umesaidia kuimarisha dhana ya utawala bora.

Pia amesema hatua hiyo imewezesha wananchi kuwasilisha malalamiko yao moja kwa moja kwa Rais na kupatiwa ufumbuzi.

Aliyasema hayo juzi wakati akiwasilisha makadirio, mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar.

Jamal alisema mtandao wa Sema na Rais Mwinyi umesaidia kufikisha malalamiko ya wananchi yanayowakabili moja kwa moja kwa Rais na kujibiwa na watendaji husika serikalini. Kwa mujibu wa Jamal, huo ni utaratibu ambao unawawezesha wananchi kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili, hivyo kujenga imani kwa wananchi kuhusu uongozi wao.

"Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba utaratibu wa kutumia mtandao 'Sema na Rais Mwinyi' kwa kiasi kikubwa umesaidia kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili wananchi, hivyo kujenga imani kubwa kwa uongozi ulioko madarakani," alisema.

Pia alisema katika kipindi cha uongozi wake, Rais Dk. Mwinyi ameanzisha utaratibu kwa waandishi wa habari kuzungumza naye kila mwezi kwa ajili ya kuuliza maswali mbalimbali yanayohusu utendaji wa kazi pamoja na mambo yanayoihusu jamii.

Alisema utaratibu huo umeungwa mkono na waandishi wa habari ambao wanatumia nafasi hiyo kuuliza maswali mbalimbali na kupatiwa majibu na Rais kwa usahihi mkubwa.

"Mheshimiwa Spika katika kujenga mahusiano (uhusiano) mazuri (mzuri) kati ya Ikulu na waandishi wa habari, Rais Mwinyi ameanzisha utaratibu wa kuzungumzo na waandishi wa habari kila mwezi ambao lengo lake kufungua milango ya demokrasia na utawala bora," alisema.

Pia alisema katika kipindi cha mwaka mmoja tangu Rais Dk. Mwinyi alipoingia madarakani, amejenga mazingira ya amani na utulivu katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa hatua ambayo imejenga utulivu wa kisiasa na kumaliza siasa za chuki na uhasama.

Alisema kuwapo kwa utulivu wa kisiasa, kumejenga matumaini makubwa kwa wananchi pamoja na wawekezaji hatua ambayo imesaidia kufungua milango ya uwekezaji wa miradi mikubwa.

Katika hatua nyingine, Waziri Jamal alisema serikali imefurahishwa na juhudi za Diaspora katika kusaidia maendeleo ya Zanzibar pamoja na uwekezaji ikiwamo kuwashawishi wawekezaji kuwekeza Zanzibar.

Alisema kwa nyakati tofauti Diaspora wamesaidia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule pamoja na vifaa vya hospitali katika hospitali zilizoko vijijini Unguja na Pemba. Hatua hiyo, alisema imesaidia kuleta maendeleo na kupambana na umaskini.

## Watakiwa kupambana uvuvi haramu baharini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI za Uvuvi za Vijiji vya Pitanazako, Fukuchani na Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja, zimetakiwa kuondoa muhali kwa wavuvi wanaofanya uharibifu wa kimazingira katika maeneo ya hifadhi za bahari.

Ofisa Mipango kutoka Idara ya Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari Zanzibar, Mchanga Khamis Said, alisema hayo alipokuwa katika kikao na kamati za uvuvi juu ya utoaji wa maoni ya changamoto na suluhisho lake, Mkokotoni Unguja.

Alisema uvuvi haramu bado tatizo kubwa katika maeneo ya hifadhi kwa mkoa wa Kaskazini Unguja jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za serikali na kudhoofisha mpango wa uchumi wa bluu.

Akizungumza kwa niaba ya wavuvi wenzake katika kikao hicho, Makame Juma Kibabu kutoka Kidoti, aliziomba taasisi za kiserikali kuweka ushirikiano na kamati za uvuvi juu ya ulinzi shirikishi na usimamizi wa sheria kwa wahalifu kuwekewa adhabu ambayo itasaidia kuondoa tatizo hilo.

Pia aliiomba serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kuwapatia chombo maalumu ambacho kitakuwa chini ya kamati za uvuvi kwa ajili ya doria katika maeneo ya hifadhi za bahari hususani katika maeneo ya uchimbaji wa mchanga na mawe ya bahari.

Naye Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Maeneo ya Hifadhi ya Tumbatu, Ramadhan Ali Mtumwa, aliwataka wavuvi kutafuta mbinu mbadala za ufugaji wa mazao ya baharini ili kupungua wimbi la wavuvi katika bahari.

Aidha, aliiomba serikali kutoa elimu kwa wavuvi kuhusu athari za uvuvi haramu unavyoathiri katika maeneo ya matumbawe na rasilimali zingine zilizomo katika bahari.



Mkuu wa Wilaya ya Magharib A Unguja, Suzan Peter Kunambi, akizungumza jana, wakati akifungua mdahalo wa majadiliano ya usalama wa waandishi wa habari na uhusiano wa Jeshi la Polisi Zanzibar, ulioandaliwa na klabu ya waandishi wa habari Zanzibar (ZPC). Kushoto ni Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Said Kificho na Katibu wa ZPC, Mwinyimvua Nzukwi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# DC ahimiza ushirikiano wa wanahabari, Jeshi la Polisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Magharibi A Unguja, Suzan Peter Kunambi, amesema ushirikiano wa pamoja katika ya vyombo vya ulinzi na usalama na waandishi wa habari utasaidia kuheshimiwa kwa uhuru wa vyombo vya habari na waandishi kufanya kazi zao kwa weledi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa majadiliano wa usalama kwa waandishi wa habari ulioandaliwa na Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) uliofanyika kituo cha huduma na sheria, Kijangwani mjini Zanzibar.

Alisema jamii inahitaji kupata taarifa kutoka kwa waandishi wa habari, hivyo si vyema waandishi kuonekana maadui na badala yake kupewa ushirikiano wanapohitaji kupata taarifa.

Mkuu huyo wa wilaya ambaye kitaaluma ni mwandishi wa habari, alisema vyombo vya ulinzi na usalama hasa Jeshi la Polisi ni chanzo kikubwa kinachotegemewa na waandishi wa habari katika kupata taarifa mbalimbali kwa ajili ya kutoa taarifa kwa jamii.

"Jeshi la Polisi ndilo linalotoa taarifa za ajali ikiwamo moto na matukio mengine ya kiusalama, hivyo niwaombe wanahabari kutumia chanzo hiki vizuri," alisema.

Kwa mujibu wa Kunambi, wako watu ambao wanatumia matukio yanayojitokeza katika jamii zikiwamo ajali kama chanzo cha habari na kutuma katika mitandao ya kijamii jambo ambalo ni kinyume cha maadili ya uandishi wa habari.

Alisema ni wajibu kwa waandishi wa habari kutafuta vyanzo sahihi vya habari na haipendezi kutumia vyanzo vizisivyo sahihi na kusisitiza kuwa Jeshi la Polisi liwe tayari pale panapojitokeza matukio makubwa katika kutoa taarifa sahihi ili kuepusha kutolewa taarifa ambazo si sahihi.

Pia aliwataka kuacha kufanya kazi kwa visasi na vinyongo na midahalo hiyo inalengo la kuondosha mambo hayo kwa sababu vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na vyombo vya habari vinategemeana katika kudumisha amani ya nchi.

Aliwasisitiza washiriki wa mdahalo huo kufanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni, miongozo, maadili ya kazi zao na uweledi ili kujiepusha na matatizo na migogoro isiyokuwa ya lazima kati ya wanahabari na vyombo vya ulinzi na usalama.

Sambamba na hilo, aliwataka kutumia mjadala huo vizuri ili kuwa chachu ya kuongeza mashirikiano kati wa waandishi wa habari na vyombo vya ulinzi na usalama vilivyoko nchini.

Naye Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Said Mohammed Said, alisema ibara ya 18 ya Jeshi la polisi imewatambua wanahabari, hivyo uhusiano kati ya polisi, vyombo vingine vya ulinzi na usalama na wanahabari hauepukiki kwa sababu wote wanaitumikia jamii moja.


# HABARI PICHA



Rais Samia Suluhu Hassan akitoka katika Msikiti Mkuu wa BAKWATA, Kinondoni Muslim, baada ya kushiriki Swala ya Eid El Fitr, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Tanga, Ummy Mwalimu, akisalimiana na mmoja wa waumini wa dini ya kiislamu, baada ya Swala ya Eid El Fitr, kwenye Msikiti Mkuu wa Ijumaa, jijini Tanga jana. **PICHA: OSCAR ASSENGA**



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaid Ally Khamis (katikati), akimkabidhi fedha kwa Ofisa Mfawidhi wa Makazi ya Wazee Nunge, Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, Jacqueline Kinyemezi, kununua vitu kwa ajili ya Sikukuu ya Eid El Fitr. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatuma Almas Nyangasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Abubakar Bin Zubeir, aliposhiriki Swala ya Idd El Fitr, iliyosaliwa kitaifa katika Msikiti wa Mfalme, Muhammad wa Sita wa Morocco, Kinondoni, Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**



Waumini wa dini ya kiislam mjini Iringa, wakishiriki Swala ya Eid El Fitr katika Uwanja wa Samora jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Waumini wa dini ya kiislamu mjini Shinyanga, wakishiriki swala ya Eid El Fitr, katika viwanja vya Sabasaba jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

HABARI KIMATAIFA

## Wanaharakati waandamana kudai haki utoaji mimba

**Washington,** MAREKANI

WANAHARAKATI wanaopinga na waoungana mkono haki ya kutoa mimba, wameandamana leo mjini Washington baada ya taarifa kwamba mahakama ya juu nchini humo inalenga kubatilisha uamuzi wa mwaka 1973.

Uamuzi huo ulioruhusu utoaji wa mimba. Rasimu ya nyaraka ya mahakama iliyovuja imeonyesha idadi kubwa ya majaji wa mahakama ya juu, wameunga mkono kubatilisha uamuzi wa kesi maarufu ya Roe dhidi ya Wade, iliyoweka msingi wa kikatiba wa haki ya kutoa mimba nchini Marekani.

Saa chache tangu kusambaa kwa taarifa hizo wanaharakati wanaounga mkono pande tofauti walikusanyika nje ya majengo ya mahakama ya juu kupaza sauti.

Kwa zaidi ya nusu karne, utoaji wa mimba limekuwa moja ya suala tete na linalogawa maoni ya umma wa Wamarekani kati ya jamii za kihafidhina na zile za kiliberali. **DW**




## Magenge yenye silaha yatumia raia kiuhalifu

**Lagos,** NIGERIA

MAGENGE yenye silaha ambayo yamewateka nyara maelfu ya abiria katika shambulizi la kwenye treni, Kaskazini mwa Nigeria yanatumia raia kama ngao ya kibinadamu na hivyo kufanya iwe vigumu kwa jeshi kutekeleza kazi ya uokoaji, Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari, amesema.

Shirika la Reli Nigeria, lilisema mwezi uliopita kuwa watu 168 walipotea kutokana na shambulizi la Machi 28, mwaka huu.

Vyombo vya habari nchini humo wiki iliyopita vilionyesha video ya waathirika wa utekaji nyara huo, akiwamo mtoto aliyezaliwa hivi karibuni na mmoja wa wanawake waliotekwa nyara. **VOA**

# Papa: Nitakutana na Putin ana kwa ana

**Vatican City,** VATICAN

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis amesema amejitolea kusafiri hadi Moscow kukutana na Rais wa Russia, Vladimir Putin, kujadili kuhusu mgogoro kati yake na Ukraine.

Papa aliliambia gazeti la Italia la Corriere della Sera, kwamba alituma ujumbe kwa Kremlin siku 20 baada ya uvamizi wa Russia, kupitia mwanadiplomasia mkuu wa Vatican.

Ni mara ya kwanza kwa Papa kuitaja Russia au kumtaja hadharani Putin tangu kuanza kwa vita nchini Ukraine zaidi ya miezi miwili iliyopita.

**Baba mkuu hawezi kujigeuza kuwa kijana wa madhabahu ya Putin.**

Papa Francis, pia alisema hivi karibuni aliwasiliana kupitia simu ya zoom ya dakika 40 na mkuu wa Kanisa la Orthodox la Urusi, Baba Mkuu Kirill anayeunga mkono vita, na alitumia dakika 20 za kwanza za simu hiyo kuelezea uhalali wake.

"Baba mkuu hawezi kujigeuza kuwa kijana wa madhabahu ya Putin," Papa alisema.

Russia yapanga kuchukua miji zaidi. Walinzi wa kiwanda cha chuma cha Azovstal kilichoko katika jimbo la Mariupol, wanasema vikosi vya Russia vinatumia ndege zisizo na rubani, vifaru na meli za kijeshi kushambulia kiwanda hicho.

Umoja wa Mataifa (UN) na Shirika la Msalaba Mwekundu wanatarajia kusimamia uokoaji wa kundi la raia watakaokimbia mapigano hii leo.

Juzi, kulikuwa pia na shambulio la roketi katika mji wa bandari wa Kusini wa Odesa.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, alielezea upinzani wa Ukraine dhidi ya uvamizi wa Russia kama kipindi bora zaidi nchini Ukraine katika hotuba yake kwa bunge.

Aliwahutubia wabunge, jana, anatarajiwa kuwasilisha maelezo zaidi kuhusu msaada wa ziada wa paundi milioni tatu kusaidia jeshi la Ukraine.

Bunge la Uingereza lilisema usaidizi wa kijeshi utajumuisha salaha za kielektroniki, mifumo ya mawasiliano na vifaa vya kusaidia kuona mbali nyakati za usiku. **BBC**



Wanafamilia wakifarijiana, huku mapigano makali yakiripotiwa katika mji wa Bandari wa Odessa na miji mingine Mashariki mwa Ukraine, wakati hatua za kuondoa raia kadhaa kutoka mji unaoshambuliwa zaidi wa Mariupol zikitarajiwa kuanza. **PICHA: DW**

# Kiwanda chanjo ya corona chakosa wateja A. Kusini

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

KIWANDA cha kwanza cha kutengeneza chanjo za corona huenda kikalazimika kufunga shughuli zake za utengenezaji wa chanjo, kutokana na ukosefu wa wateja.

Kampuni hiyo ya dawa iitwayo Aspen Pharmacare, ambayo imekuwa ikitengeneza chanjo ya Johnson & Johnson katika jimbo la Mashariki mwa Afrika Kusini la Cape, sasa inakabiliwa na hatari ya kufunga shughuli zake.

Hii inakuja wakati sehemu kubwa ya watu wa Afrika wakiwa bado hawajachanjwa.

Prof. Tulio de Oliveira, Mkurugenzi wa Kituo cha kushughulikia Majanga na Uvumbuzi Afrika Kusini, amesema kufungwa kwa kiwanda hicho kunaweza kuathiri utengenezaji wa chanjo nyingine ambazo haziathiri mataifa yaliyoendelea duniani pamoja na maandalizi kwa ajili ya magonjwa mengine ya majanga.

Alisema ubaguzi wa rangi wa chanjo umeharibu upokeaji wa chanjo za Uviko-19 katika Afrika Kusini na maeneo mengine ya bara hilo.

"Kile ambacho kilishangaza ni kwamba mwaka jana ilikuwa ni vigumu kwetu kupata chanjo...chanjo zilikuwa haziji Afrika Kusini na Afrika, lakini wakati nchi nyingine zilikuwa zimewachanja watu wake tulipata kinyume, tulipata chanjo zilizotupwa.

"Tulipata mamilioni na mamilioni ya dozi...baadhi yake muda wa kutumika ulikuwa mfupi sana kabla ya kuharibika," alisema profesa huyo.

Alisema kuwa kutokana na




kwamba Afrika ilikuwa imepitia mawimbi matatu makuu ya maambukizi ya ugonjwa huo, ikiwa ni pamoja na wimbi baya sana bila chanjo, ilikuwa imepunguza upokeaji. **BBC**

HABARI MICHEZO

# DTB KUPANDA LIGI KUU JUMAPILI

**Na Adam Fungamwango**

IWAPO itashinda kwenye mechi yake ya Jumapili dhidi ya Pamba FC, Timu ya DTB itakuwa imepanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu ujao.

DTB inahitaji pointi mbili tu kuweza kutinga Ligi Kuu, huku ikiwa imebakisha pia mechi tatu ili imalize mechi zake 30 za msimu huu.

Hata hivyo, timu hiyo inayocheza Ligi ya Championship huku ikiwa imesajili wachezaji wengi wa ndani ya nje ya nchi waliowahi kucheza Ligi Kuu, ina nafasi kubwa ya kushinda mechi hiyo ili kufanikisha hilo.

**Kama itatoka sare au kufungwa itasubiri mechi zingine mbili il izobaki.**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DTB, Muhibu Kanu, amesema kuwa lengo la kubwa si tu kuona inacheza Ligi Kuu, bali inacheza Ligi Kuu kwa mafanikio makubwa.

"Nawaomba mashabiki wa DTB, Jumapili wajazane kwenye Uwanja wa Uhuru kuishangilia timu yao, kwani kama tukishinda ni wazi moja kwa moja tunakuwa tumetinga Ligi Kuu," alisema Muhibu.

Timu hiyo inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 62, ikifuatiwa na Ihefu ambayo nayo inajaribu kutaka kurejea Ligi Kuu baada ya kushuka msimu uliopita, ina pointi 59, huku timu nyingine inayopigania kupanda moja kwa moja Ligi Kuu, au kucheza hatua ya mtoano, Kitayosce ina pointi 54, huku JKT Tanzania ambayo pia ilishuka msimu uliopita ikiwa na pointi 47.

DTB ina wachezaji kama Amissi Tambwe aliyewahi kuzichezea timu za Simba na Yanga, Waghana Nicolaus Gyan na James Kotei waliowahi kuichezea Simba, Juma Abdul aliyewahi kuichezea Yanga na wengineo wengi.

# *TADA yaomba udhamini kushiriki mashindano*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Chama cha Mchezo wa Darts Tanzania (TADA) kimeomba wadhamini kujitokeza kusaidia timu ya Taica ya mchezo huo inayojiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Juni mwaka huu, Dar es Salaam.

Katika mashindano hayo Tanzania wanatarajiwa kuwa wenyeji wa michuano hiyo ya Afrika Mashariki yajulikano kwa jina la 'Single'.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa TADA, Redmpta Mwabesa, alisema katika mashindano hayo yatashirikisha mataifa matatu ikiwamo Tanzania wenyeji, Kenya na Uganda.

Alisema michuano hiyo itashirikisha mchezaji mmoja mmoja kulingana na aina ya mchezo huku wachezaji wa Tanzania wakifanya mazoezi katika klabu zao.

"Wachezaji waliochagulia kwa sasa wanafanya mazoezi katika klabu zao, kwa sababu tunasubiri fedha kuingia ili kutuwezesha kuingia kambini na kufanya maandalizi ya michuano hiyo," alisema Mwabesa.

Alisema Tanzania itakuwa na timu mbili na jumla ya wachezaji 10, wanawake wakiwa wanne na sita wanaume ambao ni Ravi Joshi, Noah Yesaya, John Mlay, Florence Antony, Revocatus Siriwa na Umaru Habibu.

Kwa upande wa wanawake ni Happiness Modoha, Mary Swalehe, Upendo Mbogo, Subira Waziri, nyota hao hawako kambini na kufanya mazoezi ndani ya klabu zao.



Wachezaji wa Yanga, Jesus Moloko na Dickson Job wakiwa kwenye mazoezi kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting utakaopigwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika. **PICHA: YANGA**

# Biashara yawaomba radhi mashabiki

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Biashara United umewaomba radhi mashabiki wao kwa kitendo cha kushindwa kulinda goli ambalo walilipata mapema na badala yake kuruhusu bao dakika za mwisho walipocheza na Mtibwa Sugar.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka mkoani Mwanza, Meneja wa Klabu hiyo, Frank Wabare alisema anaomba mashabiki wasahau kilichotokea, na badala yake wajipange kwa ajili ya mchezo ujao wa kesho dhidi ya timu ya Dodoma Jiji.

"Tunaomba radhi mashabiki wetu kwa kile kilichotokea tunafahamu wameumizwa na matokeo haya," alisema Wabare.

Alisema baada ya kutoka sare ya bao 1-1 katika mchezo huo ambayo ilisababishwa na wachezaji kukosa umakini, kocha wao mkuu ameahidi kurekebisha makosa hayo.

Alisema kwa sasa wanajipanga kukutana na timu ya Dodoma Jiji katika uwanja wao wa nyumbani.

Alisema wanaupa umuhimu mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani.

# Chaneta kuchaguana kesho

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Netiboli Tanzania (CHANETA) kinatarajia kufanya uchaguzi kesho Mei 5 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Devota Marwa alisema nafasi zinazowaniwa ni Makamu Mwenyekiti pamoja na Katibu Mkuu.

"Tunatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi hizo baada ya kura zao kupungua kwenye uchaguzi uliofanyika Oktoba mwaka jana," alisema Marwa.

Mwenyekiti huyo alisema hadi sasa wagombea 8 wamechukua fomu za kuwania nafasi hizo ambao watafanyiwa mchujo kabla ya uchaguzi huo.

Alisema viongozi watakaochaguliwa katika uchaguzi huo wana kasi kubwa ya kufanya mabadiliko ndani ya chama hicho.

## ZISIKUPITE

### LINGARD AGOMBEWA

AC Milan na Juventus wanaongoza katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29. ***(ESPN)***

### RICHARLISON KUUZWA

EVERTON watakubali ada ya pauni milioni 50 ili kumuuza mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 24 msimu huu wa joto na wana uhakika wa kupata ofa kama hiyo. ***(Football Insider)***

### RICE ANUKIA MAN

KLABU ya Manchester United iko mbioni kumsajili kiungo wa kati wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23 kutoka West Ham. ***(ESPN)***

### MARTINEZ NA LIVERPOOL

ARSENAL wameanza upya juhudi za kumsaka mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina mwenye umri wa miaka 24, Lautaro Martinez. ***(Times)***

### LAIMER AGOMBEWA

KIUNGO wa kati wa RB Leipzig na Austria, Konrad Laimer mwenye umri wa miaka 24 analengwa na Tottenham na Liverpool, pamoja na Bayern Munich. ***(Kicker)***

### SAVIC AWANIWA

KIUNGO wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 27 huenda akajiunga na Manchester United au Paris St-Germain. ***(90min)***

### KLAVIN ABANIWA MKATABA

LEEDS United hatampatia ofa ya mkataba mpya, kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26. ***(Star)***

### DUMMETT KUSAINI

MLINZI wa Newcastle United, Paul Dummett mwenye umri wa miaka 30 anajiandaa kutia saini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Sun)***

### BERGWIJN ATAKIWA AJAX

KLABU ya Ajax itafufua tena mpango wa kumsaka mshambuliaji wa Tottenham na Uholanzi, Steven Bergwijn baada ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24 kusema yuko tayari kuondoka klabu hiyo. ***(Times)***


### AARONS KUUZWA

KLABU ya Norwich ambao imeshuka daraja inataka kumuuza mlinzi wake, Max Aarons mwenye umri wa miaka 22, msimu huu wa joto. ***(Telegraph)***

### TRAORE BASI BARCA

BARCELONA haitamsajili kwa mkataba wa kudumu, winga wa Wolves, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania kwa sasa anaichezea klabu hiyo ya La Liga kwa mkopo. ***(Marca)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RANGNICK: MAN UNITED INAHITAJI WACHEZAJI

Asema ili kushinda mataji lazima wasajiliwe wachezaji wa kiwango bora na...

**MANCHESTER,** England

RALF Rangnick ana imani kuwa Manchester United inaweza tena kuwania mataji makubwa, lakini tu kama watasajili "wachezaji bora."

**Mashetani Wekundu hao wanamaliza msimu wa tano bila taji lolote na wanakaribia kukosa kuingia katika nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu ya England.**

United walio katika nafasi ya sita waliwafunga Brentford 3-0 Jumatatu, ingawa wamepitwa pointi tano nyuma ya Arsenal katika kuwania kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na kocha huyo wa muda Rangnick anakubali kwamba biashara kubwa inahitajika ikiwa United wanataka kufikia kiwango kikubwa na wapinzani kama Liverpool na Manchester City.

Rangnick, ambaye nafasi yake itachukuliwa na Erik ten Hag mwishoni mwa msimu huu, aliiambia Sky Sports: "Ni dhahiri kwamba wachezaji wachache wataondoka na kunahitajika wachezaji wa ubora wa hali ya juu.

"Ninaamini kabisa kuwa kila mmoja akifanya kazi kwa pamoja tunaweza kuirejesha Manchester United pale tunapohitaji. "Klabu nyingine zilihitaji madirisha mawili au matatu tu ya uhamisho wa wachezaji ili kutoa changamoto, lakini kuanzia sasa tunahitaji kuleta wachezaji wa kiwango cha hali ya juu ambao wataisaidia timu.

"Ikiwa hii itatokea, sidhani kama inapaswa kuchukua muda mrefu sana."

Alipoulizwa ikiwa kama hajazungumza na bosi anayekuja Ten Hag, ambaye bado anainoa Ajax, Rangnick aliongeza: "Hadi sasa hatujaweza kuzungumza chochote."

"Lengo la Erik ni kushinda Ligi ya Uholanzi, lengo letu lilikuwa kwenye michezo yetu."

United walipata ushindi huo dhidi ya Brentford shukrani kwa mabao ya Bruno Fernandes na Raphael Varane na penalti ya Cristiano Ronaldo.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,224

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 2.89
X | 3.66
2 | 2.17

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# REAL MADRID KUIVAA MAN CITY BILA ALABA



**MADRID,** Hispania

BEKI wa Real Madrid, David Alaba hakufanya mazoezi na kikosi hicho Jumatatu, jambo lililotia shaka kama ataweza kuwa kwenye mchezo dhidi ya Manchester City, leo Jumatano.


Alaba, ambaye ameongeza taji la LaLiga kwenye mataji yake 10 ya Bundesliga baada ya Madrid kunyakua ushindi wao wa nyumbani Jumamosi, alishindwa kufanya mazoezi na kikosi hivyo kujifua peke yake.

Beki huyo mahiri, aliyesajiliwa kwa uhamisho huru msimu uliopita baada ya kumalizika kwa mkataba wake Bayern Munich, amekuwa na mchango mkubwa katika safu ya ulinzi ya Kocha Carlo Ancelotti msimu huu na amecheza mechi 45 katika michuano yote.

Hata hivyo, Alaba alitolewa katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya City wiki iliyopita, ambao walimaliza wakiwa wamefungwa 4-3. Taarifa zaidi zinasema kuwa alikuwa na tatizo la misuli ya paja, na haijafahamika iwapo atarejea kwa wakati, huku pia alikosa mchezo dhidi ya Espanyol, Jumamosi.

Madrid wanawania nafasi ya kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakayofanyika Mei 28 mjini Paris.

Gareth Bale pia hakushiriki mazoezi kamili, huku Eden Hazard akiendelea kupata nafuu kutokana na jeraha lake la kifundo cha mguu.



## Eriksen kubakia Brentfor

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Brentford, Thomas Frank anaamini "wana nafasi nzuri sana" ya kumbakisha Christian Eriksen katika klabu hiyo zaidi ya msimu huu.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Denmark mwenye umri wa miaka 30, alijiunga na nyuki hao mkataba wa miezi sita Januari.

"Siku zote nina matumaini," alisema Frank kuhusu kumbakisha Eriksen.

Tottenham, Newcastle na Manchester United ni miongoni mwa klabu zinazohusishwa na Eriksen.

Lakini Frank aliongeza: "Siku zote naamini tuna nafasi nzuri sana. Najua ana furaha hapa, anafurahia soka lake. Ni uamuzi ambao utachukuliwa mwishoni mwa msimu."

Eriksen alianza tena uchezaji wake akiwa na Brentford baada ya kuzimia alipokuwa akiichezea Denmark kwenye Euro 2020 msimu uliopita wa joto.

Amewekewa kifaa cha pacemaker, baada ya kupatwa na mshtuko wa moyo.

Eriksen amekuwa mchezaji bora wa Bre ford na ndiye al shinda katika mechi kati ya nane alizoche huku mingine ikit sare dhidi ya Tottenh na kisha kupoteza matatu kwenye Uwa wa Old Trafford dhid Manchester United.

Eriksen pia alifu katika ushindi wa dhidi ya Chelsea Ap 2.

Alipoulizwa j Brentford anajar kumshawishi ab Frank alisema: "Ra sana, ninazungur naye. Tunawasilisha pango yetu na kuija kwa pamoja."

## HABARI MICHEZO

# LIGI YA SOKA UFUKWENI YACHANJA MBUGA

Na Saada Akida

LIGI ya mchezo wa mpira wa miguu ya ufukweni inaendelea leo na Mei 8, mwaka huu kutafuta timu nne za kundi B, zitakazoungana na timu tano kwa ajili ya kucheza hatua ya nane bora ya ligi hiyo.

**Mechi zitakazochezwa leo ni mbili za kundi B ambazo ni Mshikamano City dhidi ya Kissa FC na mchezo mwingine ni Msasani Mabingwa wakivaana na Sayari FC katika Uwanja wa Fukwe za Coco, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, mratibu wa ligi hiyo, Joel Balisidya alisema tayari kuna timu tano ambazo zina nafasi ya kucheza hatua ya nane bora ya kundi B na kusubiri timu nne kutoka kundi hilo.

Alisema timu hizo nne zitapatikana katika mchezo wa leo kwa mechi mbili na Mei 8, mwaka huu wanamaliza mzunguko wa kutafuta timu mbili zingine zitakazoungana na timu zilizofanikiwa kuingia katika hatua ya nane bora.

"Hadi sasa raundi ya pili imeshachezwa na bado timu nne ambazo tunatakiwa kucheza hatua ya nane bora, kulingana na msimamo wa ligi inaonyesha jinsi gani timu zilivyojipanga na kuonyesha ushindani," alisema Joel.

Katika msimamo wa Kundi A, Friends of Mkwajuni wanaongoza wakiwa na pointi 21, Ilala FC alama 15, PCM Buza FC wakiwa na pointi 13, Savannah FC wamejikusanyia pointi12 sawa Vingunguti Kwanza na Dar es Salaam Football Centre wanashika mkia kwa alama 3 wote wakicheza michezo tisa ya ligi.

Kundi B anayeongoza ni Kijitonyama Sand Heroes kwa alama 21 pointi sawa na Kisa FC nafasi ya pili, Mburahati FC akiwa na alama 18 sawa na Msasani Mabingwa, Friends Rangers akikusanya pointi 15, Sayari FC mwenye alama tatu na Mshikamano City akiburuza mkia akiwa amepoteza michezo tisa aliyocheza.



# Revina kurudi kwenye ngoma za asili

Na Sabato Kasika

BAADA ya kimya cha muda mrefu, msanii wa ngoma za asili, Revina Kasabila, amesema kuwa sasa anajiandaa kuibuka akiwa na vibao vipya ambavyo anaamini vitamrudisha kwenye chati.

Akizungumza na gazeti hili jana, Revina alitaja baadhi ya vibao hivyo kuwa ni 'Abazaile, Abashaija' ambavyo ameimbwa kwa lugha ya Kihaya na kingine alichokipa jina la 'Wana Senene'.

"Mara ya mwisho kusikika ni kati ya mwaka 2019 au 2020 nikitamba na wimbo wa 'Tembelea Kagera', lakini baadaye nikakumbana na changamoto ambazo ziko juu ya uwezo wangu ikabidi nisimame," amesema Revina.

Revina amesema, kwa sasa ameamua kuandaa nyimbo za kutosha kabla ya kutoa albamu mpya ambayo anategemea iwe na nyimbo nane au 10 kama mipango yake itakwenda kulinga na jinsi alivyopanga.

Msanii huyo anaongeza kuwa muziki wa asili kwa sasa umekuwa nyuma baada ya wasanii kutosikika kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, kutokana na sababu mbalimbali zilizochangia muziki kwa ujumla kuyumba.

"Kama unakumbuka, mie nilitamba sana akiwamo pia Saida Karoli na wengine kadhaa kutoka mkoa wa Kagera, lakini sasa tumekuwa hatusikiki, hali inayosababisha muziki wa asili kuonekana umepotea," amesema.

Amesema kuwa anajipanga kuja upya ili kuhakikisha harudi tena nyuma, kwa madai kwamba bado ana nia ya kuendelea kusimamia muziki huo hasa kwa kuomba nyimbo zenye vionjo vya asili ya mkoa wa Kagera.

"Bado ninaendelea kudumisha mila na utamaduni wa mkoa huo, kwani wimbo wangu wa 'Senene' niliowahi kuimba umesaidia kuwafanya watu wengi kuzipenda senene ambazo ni maarufu mkoani kwetu," amesema.


4,601,040

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/05/22 | 17:00 | Burnley vs Aston Villa | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 02. 07/05/22 | 17:00 | Brentford vs Southampton | 2.21 | 3.37 | 3.02 |
| 03. 07/05/22 | 19:00 | Sassuolo vs Udinese | 2.25 | 3.56 | 2.82 |
| 04. 07/05/22 | 19:30 | Brighton vs Manchester Utd | 2.62 | 3.21 | 2.58 |
| 05. 07/05/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Mainz | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 06. 07/05/22 | 20:00 | Benfica vs Porto | 2.74 | 3.43 | 2.39 |
| 07. 08/05/22 | 16:00 | Leicester vs Everton | 2.31 | 3.22 | 2.97 |
| 08. 08/05/22 | 16:00 | Venezia vs Bologna | 2.93 | 3.27 | 2.31 |
| 09. 08/05/22 | 17:15 | Villarreal vs Sevilla FC | 2.30 | 3.25 | 3.05 |
| 10. 08/05/22 | 17:45 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.41 | 3.62 | 2.58 |
| 11. 08/05/22 | 19:00 | Salernitana vs Cagliari | 2.35 | 3.26 | 2.87 |
| 12. 08/05/22 | 19:30 | Espanyol vs Osasuna | 2.59 | 3.14 | 2.74 |
| 13. 08/05/22 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.37 | 3.30 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 04/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3368 | Bucheon vs Busan I Park | 1.97 | 3.21 | 3.55 |
| 13:15 | 2396 | Gold Coast United vs Brisbane Roar Youth | 2.37 | 3.75 | 2.43 |
| 13:30 | 1223 | Gimpo Citizen vs Gwangju | 4.08 | 3.31 | 1.81 |
| 14:05 | 1840 | Perth Glory vs Melbourne City | 7.96 | 5.17 | 1.32 |
| 16:00 | 1493 | KF Gjilani vs KF Drita | 1.56 | 3.54 | 5.63 |
| 16:00 | 2992 | Ruvu Shooting vs Young Africans | 6.04 | 3.36 | 1.57 |
| 16:00 | 3035 | KF Dukagjini vs KF Ulpiana | 1.41 | 4.18 | 6.61 |
| 16:00 | 5334 | Juventus Youth vs Empoli Youth | 1.50 | 4.26 | 5.03 |
| 16:30 | 5024 | Unirea Slobozia vs Concordia Chiajna | 3.06 | 2.77 | 2.43 |
| 16:45 | 3355 | Zira vs Gabala | 2.04 | 3.11 | 3.45 |
| 17:00 | 5488 | US Ben Guerdane vs Africain | 3.70 | 2.63 | 2.22 |
| 17:30 | 3460 | Gyirmot FC vs Paksi FC | 2.92 | 3.60 | 2.08 |
| 17:30 | 5598 | Aizawl FC vs Sudeva Delhi FC | 1.89 | 3.22 | 3.85 |
| 18:00 | 1128 | ES Sahel vs CS Sfaxien | 1.74 | 3.06 | 5.05 |
| 18:00 | 1719 | Ruzomberok vs MSK Zilina | 1.57 | 4.17 | 4.46 |
| 18:00 | 1821 | Akademija Pandev vs Shkendija | 2.68 | 2.83 | 2.68 |
| 18:00 | 3288 | Legia II Warszawa vs KS Pelikan Lowicz | 1.46 | 4.37 | 5.43 |
| 18:00 | 3915 | MTK Budapest vs Puskas Akademia | 2.96 | 3.20 | 2.22 |
| 18:00 | 3916 | Chippa Utd vs Cape Town City | 3.92 | 2.93 | 2.07 |
| 18:00 | 4028 | Baroka FC vs Golden Arrows | 2.72 | 2.91 | 2.72 |
| 18:00 | 5931 | Dziugas vs Zalgiris Kaunas | 4.39 | 3.46 | 1.72 |
| 18:30 | 3423 | Bouake FC vs ASEC Mimosas | 7.61 | 3.76 | 1.42 |
| 19:00 | 1174 | Foolad Khuzestan vs Gol Gohar | 2.70 | 2.55 | 3.20 |
| 19:00 | 2944 | Midtjylland vs Vejle BK | 1.34 | 4.48 | 7.59 |
| 19:00 | 3479 | Omonia Nicosia vs Anorthosis Famagusta | 2.17 | 3.20 | 3.06 |
| 19:00 | 4090 | FC Krasnodar vs Lokomotiv Moscow | 2.36 | 3.31 | 2.82 |
| 19:00 | 4170 | PAOK vs Olympiakos | 2.58 | 3.12 | 2.73 |
| 19:00 | 4495 | CSA Steaua Bucuresti vs Universitatea Cluj | 3.16 | 3.01 | 2.22 |
| 19:00 | 4805 | Suduva vs Vilniaus Riteriai | 2.31 | 2.93 | 3.07 |
| 19:00 | 5054 | FK Sumgayit vs Neftchi Baku | 6.22 | 3.74 | 1.49 |
| 19:00 | 5788 | Ethnikos Achnas vs AEK Larnaca | 5.05 | 3.69 | 1.58 |
| 19:10 | 4785 | Persepolis FC vs Peykan FC | 1.31 | 4.37 | 9.31 |
| 19:30 | 5177 | Ferencvaros TC vs Zalaegerszegi TE | 1.32 | 4.76 | 7.57 |
| 19:35 | 3514 | Al Orubah vs AL Nahdha | 2.05 | 2.87 | 3.79 |
| 20:00 | 1491 | Bayern Munchen II vs 1860 Rosenheim | 1.07 | 8.98 | 17.56 |
| 20:00 | 1699 | Slovacko vs Sparta Prague | 2.73 | 3.12 | 2.42 |
| 20:00 | 3181 | Zalgiris vs Banga Gargzdai | 1.08 | 8.00 | 19.51 |
| 20:30 | 2691 | Maritzburg Utd vs Bloemfontein Celtic | 2.96 | 3.16 | 2.35 |
| 21:00 | 3357 | Manchester City W vs Birmingham W | 1.01 | 18.00 | 40.00 |
| 21:00 | 3969 | ND Gorica vs NK Dob | 1.35 | 4.38 | 7.59 |
| 21:15 | 2793 | Arsenal W vs Tottenham W | 1.04 | 9.53 | 29.18 |
| 21:30 | 1608 | Avellino vs Foggia | 1.78 | 3.10 | 4.66 |
| 21:30 | 2606 | Pescara Calcio vs Gubbio | 1.71 | 3.36 | 4.58 |
| 21:30 | 2720 | Virtus Entella vs Olbia Calcio | 1.73 | 3.35 | 4.47 |
| 21:30 | 3513 | Triestina vs Pro Patria | 1.98 | 3.12 | 3.65 |
| 21:30 | 4151 | Monopoli vs Virtus Francavilla | 1.91 | 3.02 | 4.09 |
| 21:30 | 4335 | Pro Vercelli vs Juventus U23 | 2.07 | 2.92 | 3.65 |
| 21:45 | 4981 | Queens Park vs Dunfermline | 3.25 | 3.05 | 2.22 |
| 22:00 | 4351 | Real Madrid vs Manchester City | 2.89 | 3.66 | 2.17 |
| 23:00 | 4278 | Llaneros FC W vs Millonarios FC | 3.36 | 3.17 | 2.06 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Mei 4, 2022
Nipashe



'Man U inahitaji wachezaji bora' UKURASA 21

BAO HILO...



Mchezaji wa Simba, Shomari Kapombe (kushoto), akifunga bao la kusawazisha dhidi ya Namungo FC wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baina ya timu hizo jana, Uwanja wa Ilulu mjini Lindi. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YAISOGEZEA UBINGWA YANGA SC

**Na Dennis Fussi**

## ●●● Ni baada ya kulazimishwa sare ya 2-2 na Namungo FC huku...

SIMBA jana ililazimishwa sare ya kufungana 2-2 na Namungo FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika Uwanja wa Ilulu mjini Lindi.

**Sare hiyo ina maana kwamba, Simba imezidi kuisogeza Yanga kwenye ubingwa wa Ligi Kuu, kwani kama ikishinda mchezo wake wa leo dhidi ya Ruvu Shooting itaongeza pengo la pointi baina yao.**

Simba baada ya mchezo huo imefikisha pointi 43 ikishuka dimbani mara 21, huku Yanga (kabla ya mchezo wa leo) ina pointi 53 wakiwa wanaongoza kwa tofauti ya pointi 12.

Katika mchezo huo, dakika tano za kwanza, Simba waishambulia lango la Namungo FC kwa kasi, lakini umakini mdogo wa wachezaji wake, Medie Kagere, Kibu Dennis na Peter Banda ukawafanya washindwe kufunga.

Namungo walijibu mashambulizi wakati mshambuliaji wao David Molinga alipomzidi maarifa mlinzi wa Simba, Josh Onyango ambaye alimfanyia faulo iliyopigwa na Haruna Shamte na ikaokolewa na golikipa Aishi Manula na kuzaa kona.

Mpira wa kona iliyopigwa na Chiza Kichuya ulitua kichwani mwa Jacob Masawe aliyefunga bao la kuongoza kwa Namungo dakika ya 7 akiwazidi akili mabeki wa Simba.

Baada ya bao hilo, Simba walifanya mashambulizi makali na kupiga mashuti matano yaliyolenga goli, lakini golikipa wa Namungo, David Kissu alikuwa imara kuokoa hatari zote.

Jitihada za Simba kulisakama lango la Namungo zilizaa matunda dakika ya 42 wakati Shomari Kapombe alipouwahi mpira na kufunga kwa shuti kati bao la kusawazisha dakika ya 42.

Timu hizo zilikwenda mapumziko zikiwa zimetoshana nguvu, huku Simba ikifanya mashambulizi mengi zaidi kwenye lango la Namungo ndani ya dakika 20 za mwisho wa kipindi hicho.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi, lakini Namungo wakapata tena bao la uongozi likifungwa na Obrey Chirwa kwa kichwa akiunganisha krosi ya Lusajo na akafunga la tatu, lakini alikuwa ameotea.

Simba walisawazisha bao hili kwa shuti la Kibu akiunganisha mpira wa kichwa uliopigwa na Kagere na hivyo kuufanya mchezo huo kumalizika kwa 2-2.

## Yanga, Ruvu mwisho wa reli

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga leo watahitaji ushindi wa aina yoyote dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma ili kufikisha pointi 58 zitakazowafanya kuingia sebuleni mwa chumba kilichohifadhiwa kombe la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati Yanga ikihitaji ushindi huo, Ruvu Shooting nayo ambayo imeupeleka mchezo huo mjini Kigoma, itakuwa inahitaji ushindi kwa hali yoyote ile ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Klabu ya Yanga imesema inauhitaji ushindi huo si tu kuukaribia ubingwa, lakini kuwapa wanachama na mashabiki wake zawadi ya sikukuu ya Idd El Fitri, huku Ruvu Shooting ikidai kama Kigoma ni mwisho wa reli, basi leo ndiyo itakuwa mwisho wa Yanga kutopoteza mechi yoyote ile.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, amesema timu yao imepata mapokezi makubwa na mazuri, hivyo cha kuwalipa ni ushindi.

"Tumefika salama na tumepata mapokezi makubwa, kwani mara ya mwisho kutuona mashabiki wa Kigoma ni kwenye fainali za Kombe la FA msimu uliopita, lakini hawakupata bahati ya kuwaona kina Fiston Mayele, Khalid Aucho na wengine na hii ilikuwa ni fursa yao kuwaona. Tumekuja kukusanya pointi tatu, tunaiombea timu yetu ipate matokeo mazuri ili tuwape wanachama na mashabiki wa timu hiyo Idd Mubarak," alisema Bumbuli.

Akizungumzia adhabu ya faini ya shilingi milioni tatu waliopigwa na Bodi ya Ligi alisema hiyo wameiona na kwa sababu fedha zao za mechi yao dhidi ya Simba zimeingia hawana wasiwasi.

"Mlango ambao tuliingilia kwenye Uwanja wa Azam Complex msimu uliopita, ndiyo huo huo tuliingilia, adhabu tumeiona, fedha zetu za mechi dhidi ya Simba zimeshaingia, tutalipa na mambo mengine yanaendelea, sisi tunatafuta ubingwa, timu ipo Kigoma, tupo vizuri," alisema.

Yanga ni moja kati ya timu iliyotozwa faini na moja kati ya kosa ni kuingia kwenye mlango usio rasmi kwenye mechi yao dhidi ya Azam FC iliyofanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Aprili 6 na kushinda mabao 2-1.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >